# CHANGAMOTO ZA KUTAFSIRI TUNGO ZENYE UTATA KUTOKA KISWAHILI KWENDA KIINGEREZA

**MWAJUMA ALI SALEH**

**TASINIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YAKUTOSHELEZA BAADHI YA MASHARTI YA SHAHADA YAUZAMILI (M.A KISWAHILI - ISIMU) YA CHUO KIKUUHURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasnifu hii iitwayo **"Changamoto za Kutafsiri Sentensi za Kiswahili Sanifu Zenye Utata kwenda Kiingereza."** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

……………………………………….

Dkt.Nestory N. Ligembe

(Msimamizi)

…………………………………

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa /shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Mwajuma Ali Saleh,** natamka kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe haijatolewa na haitotolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine ambayo ni sawa aukaribu sawa nahii katika chuo kikuu kingine.

………………………………………..

Sahihi

………………………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa mume wangu Mbarouk Salim Mbarouk  Jaji Mahakama ya Rufaa ya Tanzania pamoja na watoto wangu Hassanat, Fatma, Salim na Omar kwa mapenzi na ustahamilivu wao wakati wote wa utafiti huu. Mwenyezi Mungu aijaalie iweni familia yenye kupendana daima, AMIIN.

## SHUKURANI

Kwa kuanzia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kunipa uwezo wa kukamilisha utafiti huu. Kipekee nawashukuru marehemu wazazi wangu baba Ali Saleh Suleiman na mama Fatma Khamis Yussuf kwa kunilea katika maadili mema na kunifanya jinsi nilivyo leo hii.Ninawaenzi na ninawaombea daima, Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema AMIIN.

Kwa kiasi kikubwa ukamilishaji wa utafiti huu unatokana na msaada wa watu wengi. Nitakuwa mchoyo wa fadhila ikiwa sitatoa shukurani kwa wote walionisaidia hadi kukamilika kwake. Lakini haitokua rahisi kuwataja wote isipokuwa nitawataja wachache kwa niaba ya wengine.

Ninatoa shukurani zangu kwa msimamizi wangu wa utafiti, Dr. Nestory N. Ligembe kwa kukubali kuwa msimamizi wangu kwa kusimamia utafiti, kunielekeza, kunishauri na kunikosoa katika kipindi chotecha utafiti huu pamoja na majukumu mengi aliyonayo. Ametumia busara kunielekeza hadi kukamilika kwa utafiti huu. Bila yeye sidhani kama ningeliweza kuikamilisha kazi hii ngumu.

Pia ninawashukuru walimu na wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunifundisha kozi ya mbinu za utafiti ambayo iliniongoza katika uchambuzi wa data nilizozikusanya. Aidha, ninawashukuru wanafunzi wezangu tuliokua pamoja katika kipindi chote cha masomo kwaushirikiano makubwa tulio kuwa nao na wale wote walionipa msaada wao katika uchambuzi wa data. Pia sitamsahaumwalimu Mussa Khamis, Ahmed Ali Makame na mwalimu Ali Saleh wa Chuo Kikuu Suza kwa maelekezo yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamechangia kukamilika kwa utafiti huu.

Mwisho ninaishukuru familia yangu akiwemo mume wangu na watoto wangu kwa uvumilivu mkubwa waliouonyesha kwa kipindi chote cha utafiti huu.

## IKISIRI

Utafiti huuulilenga kuchunguza changamoto zilizopo katika kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na madhara yake katika ufanisi wa mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa lugha hizo mbili. Utafiti huu umetumia mkabala wakimaelezo na kitakwimu katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu. Utafiti huu ulifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika Wilaya ya Magharibi A na B na Wilaya ya Mjini. Mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ni tatu yaani, usomaji wa machapisho, dodoso na usaili. Aidha, utafiti huu ulitumia sampuli nasibu kuteua walengwa wa utafiti. Watafitiwa 100, ikiwa ni pamoja na wanawake50 na wanaume 50 ndio waliotumika katika utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ulinganifu wa kimuundokatika kukusanya, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti. Utafiti huu umebaini kuwa kuna tungo zenye utata katika Kiswahili. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa kuna changamoto za kutafsiri tungo tata za Kiswahili kwenda katika Kiingereza. Miongoni mwa changamoto hizo ni kukosekana kwa visawe, changamoto ya kiutamaduni, Changamoto inayotokana na tofauti za kimaeneo (lahaja), changamoto za kiisimu, kimuktadha na changamoto inayotokana na miundo ya sentensi. Vile vile utafiti huu ulibaini kuwa changamoto hizo zina athari katika mawasiliano kwa sababu husababisha upotofu wa maana na ujumbe, kupotosha muundo wa tungo za matini chanzi, kukosekana kwa ushikamani wa ujumbe na kukosekana kwa ushikamani wa matini chanzi na matini lengwa. Utafiti huu unapendekza kwamba tafiti zingine zinaweza kufanyika ili kuchunguza changamoto za kutafsiri tungo tata za lugha zingine.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ ii

**HAKIMILIKI** ........ iii

**TAMKO LA MTAHINIWA** ........ iv

**TABARUKU** ........ v

**SHUKURANI** ........ vi

**IKISIRI** ........ viii

**KIELELEZO** ........ xiii

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ xiv

**ORODHA YA VIAMBATANISHO** ........ xv

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**UTANGULIZI** ........ 1

1.1 Usuli wa Tatizo ........ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 4

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 4

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti ........ 4

1.3.2 Malengo Mahususi ........ 4

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 5

1.5 Umuhimuwa Utafiti ........ 5

1.6 Mipaka ya Utafiti ........ 5

1.7 Uzingativu wa Masuala ya Kiitikeli (Kimaadili) ........ 6

1.8 Muundo wa Tasnifu ........ 8

1.9 Vikwazo vya Utafiti ........ 8

1.10 Hitimisho ........ 9

**SURA YA PILI ..... 10**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ..... 10**

2.1 Utangulizi ..... 10

2.2 Dhana ya Tafsiri na Historia Yake ..... 10

2.3 Tafiti kuhusu tafsiri ..... 15

2.4 Dhana ya Utata, Fasili na Chanzo Chake ..... 18

2.5 Kiunzi cha Nadharia ..... 23

2.5.1 Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo ..... 23

2.6 Muhutasari ..... 26

**SURA YA TATU ..... 27**

**MBINU ZA UTAFITI ..... 27**

3.1 Utangulizi ..... 27

3.2 Usanifu wa Utafiti ..... 27

3.3 Eneo la Utafiti ..... 27

3.4 Sampuli na Usampulishaji ..... 29

3.4.1 Sampuli ya Watafitiwa ..... 29

3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data ..... 31

3.5.1 Maktaba ..... 32

3.5.2 Hojaji ..... 32

3.5.3 Mahojiano ..... 33

3.6 Mbinu za Uchambuzi wa Data na Uwasilishwaji wa Matokeo ..... 35

3.7 Muhtasari ..... 35

**SURA YA NNE ..... 36**

**UWASILISHAJI WA MATOKEO NA MAJADILIANO ..... 36**

4.1 Utangulizi ........ 36
4.2 Tungo Tata katika Lugha ya Kiswahili ........ 36
4.2.1 Sababu za Utata katika Sentensi za Kiswahili Sanifu ........ 38
4.2.2 Kubainisha Utata katika Sentesi za Kiswahili Sanifu ........ 41
4.2.2.1 Matumizi ya Maneno Yenye Maana Zaidi ya Moja ........ 41
4.2.2.2 Mofimu ya Kauli ya Utendea ........ 42
4.2.2.3 Kutozingatia Taratibu za Uandishi ........ 44
4.2.2.4 Kutumia Neno Bila Kuzingatia Mazingira au Muktadha Unaohusika ........ 45
4.2.2.5 Kuwepo kwa Kiambishi Kiwakilishi Nafsi Kiambata (–a, –wa-) ........ 46
4.2.2.6 Matumizi ya Viwakilishi –ake, oa ........ 47
4.2.2.7 Utata Unaosababishwa na Mzizi – ingine- ........ 48
4.2.2.8 Matumizi ya Baadhi ya Viunganishi ........ 49
4.2.2.9 Matumizi ya Baadhi ya Vihusishi ........ 50
4.2.2.10 Makosa ya Kisarufi na Kimantiki ........ 51
4.3 Changamoto za Kutafsiri Tungo na Athari Zake katika Mawasiliano ........ 55
4.3.1 Uwepo wa Changamoto za Kutafsiri Sentensi Zenye Utata ........ 56
4.3.2 Changamoto za Kutafsiri Sentensi Zenye Utata ........ 57
4.3.2.1 Changamoto za Tofauti za Kiutamaduni ........ 57
4.3.2.2 Changamoto za Ukosefu wa Visawe ........ 59
4.3.2.3 Changamoto za Muktadha na Mazingira ........ 60
4.3.2.3 Changamoto ya Kimuktadha na Matumizi ........ 61
4.3.2.4 Tofauti za Kimaeneo ........ 62
4.3.2.5 Changamoto ya Miundo ya Kisarufi ........ 62
4.3.3 Athari za Changamoto za Tafsiri ya Sentensi Tata katika Mawasiliano ........ 64

4.4 Muhtasari ........................................................................................................ 65

**SURA YA TANO ................................................................................................. 67**

**MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO......................................... 67**

5.1 Utangulizi........................................................................................................ 67

5.2 Muhtasari ........................................................................................................ 67

5.3 Hitimisho......................................................................................................... 68

5.4 Mapendekezo .................................................................................................. 69

**MAREJELEO........................................................................................................ 71**

**VIAMBATANISHO ............................................................................................. 74**

## KIELELEZO

Kielelezo Na. 3.1: Ramani ya Sehemu Zilizofanyiwa Utafiti.....................................28

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 3.1: Sampuli ya Watafitiwa Katika Maeneo Teule ..................................30

Jedwali Na. 4.1: Kuwepo kwa Changamoto za Kutafsiri Tungo Tata ........................56

# ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na. I:Orodha ya Sentensi Tata Katika Kiswahili Sanifu ..................74

Kiambatanisho Na. II: Maswali ya Utafiti ..............................................................79

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo

Tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo, taarifa au ujumbe wa maadishi uliomo katika lugha moja (Lugha Chanzi- LC) na kuupeleka katika lugha nyingine (Lugha lengwa – LL) kwa madhumuni ya kufanikisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lugha zinazotofautiana (Mwansoko, 2016).

Kwa mujibu wa Mwansoko (2006) tafsiri ni uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Nikuchukua mawazo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzo) na kuweka badala yake mawazo yanayolingana kutoka lugha nyingine (Lugha lengwa) (Taz. Catford, 1865:20). Aidha Mshindo (2010:20) anafafanua tafsiri kuwa ni kuhawilisha mawazo kutoka lugha chanzi (LC) kwenda lugha lengwa (LL). Mtaalamu wa tafsiri huitwa Mfasiri.Mambo ya msingi katika maana hizo hapo juu ni mawazo, lugha chanzi na lugha lengwa. Aidha tafsiri inahusu lugha ya maandishi tu na siyo lugha ya mazungumzo.

Mojawapo ya dhima za tafsiri ni kuwa, tafsiri ni njia ya mawasiliano.Kama njia ya mawasiliano, tafsiri hutumika kutolea maelezo ya kibiashara, hutumika kwenye vyombo vya habari, hutumika kwenye nyaraka rasmi, Kama mkataba, ripoti za kimataifa, Makala za kitaaluma, vitabu vya kiada na ziada. Kwa vile tafsiri ni njia ya mawasiliano, basini muhimu mawasiliano ya aina hii kufanywa kwa tafsiri sahihi. Endapo kutakuwepo nautenge katika tafsiri, basi mawasiliano hayawezi kukamilika.Tafsiri tenge inaweza kuharibu maana na ujumbe lengwa na hivyo kuvuruga mawasiliano. Kwa mfano, inasemekana mlipuko wa bomu la atomiki ya

huko Japani ulisababishwa na tafsiri tenge ya neno la Kijapani “MOKASUTU” katika simu ya maandishi (telegramu) iliyopelekwa Washington D.C kutoka Japani Neno hilo lilitafsiriwa kwa makosa kuwa “Ignore” badala ya “Considered” (Mwansoko, 1996:2).

Tafsiri huhusisha lugha, kama inavyoelezwa na wataalamu, lugha zote duniani hutofautiana katika misingi ya kiisimu kama vile kanuni, miundo, maana na uamilifu wake. Kiswahili naKiingereza ni lugha mbili zenye kutofautiana kiisimu, kiutamaduni na kimuktadha (taz. Jilala, 2014). Kwa maana hiyo, lugha hizi zina kanuni na sifa tofauti. Lugha ya Kiswahili ina maneno ambayo yanapotumika katika tungo huwa na maana tata na sentensi hizi tunaziita tungo tata kwa sababu huwa na maana zaidi ya moja. Sentensi kama hizi huhitaji tafakari na uhusishaji wa muktadha ili kupata maana zake. Masebo na Nyangwine (2009) wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ina maneno yenye fahiwa zaidi ya moja.

Ili kuainisha tofauti za fahiwa, wakati mwingine hutegemea matamshi au mazingira ya matumizi ya neno linalohusika. Akishadidia mawazo hayoMatinde (2012) anasema kuwa, ni vigumu kufasili maana ya maana ya maneno kwa sababu ya kufungamana na sifa za” homonimia” ambapo kuna baadhi ya maneno yanayorejelea zaidi ya hali au kitu kimoja. Swali la kujiuliza ni je, maneno ama sentensi hizi zinatafsiriwavipi? Ikumbukwe kwamba, lengo kuu la lugha yoyote ni kuwezesha mawasiliano baina ya wasemaji wa lugha hiyo.Mawasiliano yenye ufanisi hayakamiliki ikiwa tafsiri iliyofanywa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine inashindwa kuhawilisha mawazo yenye maana sahihi iliyokusudiwa kwenye matini ya lugha chanzi.

Kwa hiyo, swali la kujiuliza katika utafiti huu ni namna gani tunaweza kutafsiri sentensi zenye utata kutoka katika lugha moja kwenda katika lugha nyingine? Ni changamoto gani ambazo mfasiri wa sentensi zenye utata anaweza kukumbana nazo anapotafsiri sentensi zenye utata kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza? Tafsiri ya sentensi zenye utata huweza kukabiliwa na changamoto katika tafsiri, hii ni pamoja na kuzalisha tafsiri tenge ya mawazo kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha nyingine. Kwa sababu hiyo, msomaji wa matini ya lugha lengwa ya Kiingereza huweza kuhawilisha maana isiyo kusudiwa katika matini ya lugha chanzi kwa vile tungo tata huwa na maana zaidi ya moja, mfasiri anaweza kuteua visawe ambavyo si mwafaka wakati wa kutafsiri na hivyo kuzalisha maana na ujumbe usio sahihi. Matokeo ya tafsiri hii ni kutokukamilika kwa mawasiliano baina ya msemaji wa lugha chanzo na yule wa lugha lengwa.Ni dhahiri kwamba upo uwezekano mkubwa wa kuwepo tatizo la kukosekana kwa mawasiliano yenye ufanisi baina ya matini chanzi na matini lengwa kutokana na tafsiri tenge ya tungo tata za lugha ya Kiswahili sanifu zinapotafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.

Kwa sababu hiyo tuliona kuna haja ya kufanya utafiti wa kuchunguza changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kwa hiyo utafiti huu ulikusudia kuchunguza changamoto za kutafsiri tungo zenye utata za lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza. Lengoni kubaini athari za kimawasiliano zitokanazo na tafsiri ya sentensi tata kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza. Kwa kufanya hivi tunaweza kubaini namna bora ya kukabiliana na sentensi zenye utata katika lugha wakati wa kuzitafsiri kutoka katika lugha moja kwendakatika lugha nyingine.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu changamoto na matatizo ya tafsiri za Kiswahili katika nyanja mbalimbali na kwa kutumia mikabala na nadharia tofauti tofauti (taz.Batibo 1989, Bwenge 1999, Mutasa 1999,Mtui 2009, Malangwa 2005 na 2010, Jilala, 2014, 2016 na 2017). Hata hivyo, watafiti hao hawakujiegemeza katika kuchunguza changamoto za kutafsiri sentensi tata za Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utakuwa na lengo kuu na lengo mahususi.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu nikuchunguza changamoto za kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza na athari zake katika mawasiliano yenye ufanisi baina ya wazungumzajiwa lugha hizo mbili.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

(i) Kubainisha tungo tata za lugha ya Kiswahili na tafsiri yake katika lugha ya Kiingereza.

(ii) Kubainisha changamotoza kutafsiri tungo tata zalugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza.

(iii) Kubainisha athari za changamoto katika kutafsiri sentensi tata za Kiswahili kwenda Kiingereza katika mawasiliano.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo:

(i) Tungo tata za lugha ya Kiswahili zimetafsiriwaje katika lugha ya Kiingereza?

(ii) Ni changamoto zipi zinazojitokeza katika kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza?

(iii) Ni athari zipi za kimawasiliano zinazotokana na changamoto ya kutafsiri tungo tata kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza?

## 1.5 Umuhimuwa Utafiti

Utafiti huu umetoa mchango wa maarifa mapya katika taaluma ya tafsiri kwa kubainisha changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na pia kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuzikabili sentensi zenye utata katika tafsiri. Aidha, utafiti huu umeonyesha athari za tafsiri tenge za tungo zenye utata katika mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza na wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, utafiti huu umebaini changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na namna ya kuzitatua ili kufanya tafsiri sahihi ya tungo hizo.

Pia, utafiti huu unaweza kutumika kama rejeleo na chachu ya tafiti nyingine katika fasihi nalugha. Aidha, mapendekezo ya tafiti zijazo katika maeneo ambayo utafiti huu haukuweza kuyagusa kutokana na malengo mahsusi ya utafiti huu, yatasaidia kuwapa mwongozo watafiti wengine ili kuzalisha tafiti nyingi zaidi katika lugha na fasihi.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Sentensi katika lugha ya Kiswahili zimegawanyika katika makundi mbalimbali kama vile; sentensi sahili, changamano, ambatano, shurutia na kadhalika. Aidha katika

lugha ya Kiswahili sentensi huweza kuwa tata au zenye kuleta maana ya kawaida. Utafiti huu umelenga kuchunguza tafsiri ya sentensi tata kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, utafiti huu hautajihusisha wala kushughulikia tafsiri ya sentensi za lugha nyingine, ingawa zinaweza kutumika hapa na pale kwa ajili ya urejelezi.

## 1.7 Uzingativu wa Masuala ya Kiitikeli (Kimaadili)

Hiki ni kipengele kinachohusika na masuala ya kimaadili katika utafiti na namna mtafiti alivyoweza kuyazingatia kabla ya utafiti, wakati na baada ya kukusanya data. Padgett (2002) anafafanua masuala ya kimaadili ambayo huweza kuibuka na yanayopaswa kuzingatiwa katika aina zote za utafiti. Masuala hayo ni pamoja na kuomba idhini na ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo ya utafiti, usiri, uwazi, ushiriki wa hiari kwa wahojiwa, utiifu na uvumilivu.

Utafiti huu ulihusisha watu kutoka asasi mbalimbali. Kwa vile kila asasi ina sheria, taratibu, kanuni na utamaduni wake, kabla ya kufanya utafiti, mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Huria. Kibali hicho kilimsaidia mtafiti kuingia katika maeneo ya utafiti. Kabla ya kuwaona watafitiwa, mtafiti aliwaona viongozi au watu wenye mamlaka katika maeneo husika, ili kujitambulisha na kuhalalisha uwepo wake na kubainisha shughuli alizokusudia kuzifanya akiwa katika eneo husika.

Schutt (2006) anaeleza kuwa ni muhimu sana washiriki wa utafiti wakashiriki kwa kujitolea bila kulazimishwa. Katika utafiti huu, mtafiti aliwaomba washiriki wake kushiriki kwa hiari na kwa kujitolea katika kutoa data za utafiti huu. Wahojiwa walioshiriki katika kutoa data za utafiti huu, walitoa data hizo kwa hiari na kwa

uamuzi wao bila kushinikizwa na mtafiti. Wakati wa utafiti, mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti na kwa nini anahitaji kupata data hizo, na kisha kuwaomba washiriki kikamilifu katika usaili na kujibu maswali yaliyopo kwa hiari. Hata hivyo, mtafiti alijadiliana kwanza na wahojiwa kuhusu lengo kuu la utafiti huu na matarajio yake ili kupata mawazo, maoni na mtazamo wao. Wahojiwa waliweza kutoa mawazo yao, maoni na mtazamo wao kwa kile wanachokifahamu kuhusiana na lengo kuu la utafiti huu kwa uhuru zaidi. Hii ilisaidia kurahisisha zoezi zima la utafiti na shughuli ya ukusanyaji wa data za utafiti huu.

Usiri ni suala la kimaadili ambalo mtafiti alilizingatia wakati wa kukusanya data. Speziale na Ronet, kama walivyonukuliwa na Malangwa (2010) wanasema kwamba washiriki hawanabudi kuhakikishiwa na watafiti kuwa usiri wa data wanazozitoa utazingatiwa. Hii ni pamoja na kuwahakikishia kuwa, data hizo hazitatumika vinginevyo zaidi ya kutimiza malengo ya utafiti huu na bila kubainisha chanzo cha data hizo.

Mtafiti alizingatia pia suala la usiri kwa kuwaahidi na kuwahakikishia washiriki wa utafiti huu, ambao walishiriki katika usaili kuwa, data walizozitoa zitakuwa ni siri ya mtafiti na mhojiwa na zitatumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu. Kwa kuwathibitishia hayo, wahojiwa hawakutakiwa kutaja majina yao, ili kulinda siri ya mtoa data. Vilevile katika mjadala wa matokeo haya, hakuna urejelezi wa jina uliofanywa katika uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data. Kulingana na ahadi ambayo mtafiti aliitoa kwa wahojiwa wake, data zote alizokusanya kutokana na usaili kwa kinasa sauti zimehifadhiwa kwa usiri mkubwa. Hii nimaanisha kwamba, mtafiti

alichukua tahadhari kubwa katika kuzingatia vipengele vyote vya maadili katika utafiti.

### 1.8 Muundowa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni sura tangulizi ambayo inatoa utangulizi wa jumla wa utafiti na kuibua tatizo la utafiti. Sura ya pili inachambua na kujadili mapitio ya maandiko yanayohusiana na utafiti huu na hatimaye kuibua pengo la kimaarifa ambalo ndilo lililohamasisha nia ya kufanya utafiti huu. Aidha, katika sura hii kiunzi cha nadharia kilichoongoza uchunguzi, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu kimejadiliwa. Sura ya tatu inafafanua na kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura ya nne ndiyo kiini cha utafiti huu ambapo uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data na matokeo ya utafiti huu umefanyika kwa kina. Sura ya tano inatoa muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti huu.

### 1.9 Vikwazo vya Utafiti

Kikwazo kimojawapo kilichomkabili mtafiti katika utafiti huu ni kutopatikana kwa marejeleo ya kutosha yanayohusiana na mada ya utafiti huu kwa sababu ni mada ambayo haijafanyiwa tafiti nyingi. Hata hivyo, tatizo hili halikuathiri upatikanaji wa data. Mtafiti alijitahidi kusoma machapisho yaliyohusiana kwa karibu na utafiti huu ili kujadili na kujenga hoja za data na matokeo ya utafiti huu.

Vilevile, baadhi ya watafitiwa kutokuwa tayari kufanya mahojiano na mtafiti. Watafitiwa hao wanadai kupotezewa muda na pia kuona kuwa mtafiti anapata malipo anapofanya utafiti. Pamoja na kuwa hili lilionekana kuwa tatizo lakini halikuathiri upatikanaji wa data. Mtafiti aliwaelimisha wahojiwa kwa kuwaeleza malengo ya

utafiti huu kuwa ni kitaaluma na sivinginevyo(taz. Kipengele 1.7) Kwa hiyo wahojiwa walikubali na kuonyesha ushirikiano katika kutoa data za utafiti huu.

### 1.10 Hitimisho

Sura hii imetoa utangulizi kwa kubainisha mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti uliofanyika. Mambo hayo ni pamoja na usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, uzingativu wa maswala ya kiitikeli na mpangilio wa tasnifu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imegawika katika vipengele vikuu vitatu, kipengele cha kwanza kimejadili dhana ya tafsiri, fasili na historia yake.Kipengele cha pili ni mapitio ya kinadharia. Katika kipengele cha tatu mtafiti amejadili kwa kirefu tafiti, pamoja na makala mbalimbali zinazohusina na mada ya utafiti.

## 2.2 Dhana ya Tafsirina Historia Yake

Kietimolojia dhana kufasiri imetokana na neno la Kiingereza“translation” lenye maana ya kupeleka upande wa pili au kuleta upande wa pili. Catford (1965), naye amefasili tafsiri kuwa ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi) na kuweka badala yake mawazo yanayolingana kutoka lugha nyingine (lugha lengwa).

Kwa upande wao Nida naTarber (1969)wanaeleza kuwa kutafsiri hujihusisha na kuhamisha ujumbe katika lugha lengwa ambao ni linganifu kutokana na ule wa lugha chanzi kwa kuzingatia maana na mtindo.Newmark (2003:5) ameeleza kuwa kufasiri ni kuweka maana ya matini moja katika lugha nyingine kwa namna ambayo mwandishi amekusudia matini hiyo iwe.

Catford (1965) anafasili tafsiri kuwa ni mchakato wa uhawilishaji wa mawazo au ujumbe wa maneno kutoka katika lugha ya matini chanzi na kuweka ujumbe au mawazo yanayolingana na hayo katika lugha ya matini lengwa.

Batibo (1984) anajadili matatizo ya kimuundo na kisemantiki ambayo humkabili mfasiri wa lugha moja kwa nyingine. Katika kufafanua mwenendo wa tafsiri na mbinu zake, ameonesha matatizo yanayochangia upungufu katika kazi za tafsiri. Kwa mfano Batibo ameeleza, upungufu wa tafsiri ya kisemantiki ni kwamba haiwekei maanani misemo au nahau maalumu inayohusiana na utamaduni wa misimamo ya lugha lengwa katika tafsiri.

Kwa hivyo anashauri kwamba mfasiri awe huru kutafuta maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali za utamaduni na mazingira ya lugha lengwa na kusema kuwa pindi mfasiri hatayazingatia haya tafsiri yake itakuwa pungufu. Kazi ya Batibo (1984) imemsaidia mtafiti kubainisha tafsiri ya sentensi tata za Kiswahili kwenda Kiingereza kwa kuonesha maana zaidi ya moja zinazopatikana katika sentensi za lugha ya Kiswahili sanifu. Gouadec (2007) anafafanua kwamba uhamishaji huo hasa ndilo jukumu kuu la mchakato mzima wa kutafsiri na ndilo linalotekelezwa na wafasiri. Uhamishaji, au kama Mwansoko na wenzake (2006) wanavyouita "uhawilishaji" unamaanisha usafirishaji wa maudhui na maana sio tu kutoka lugha moja (L1) kwenda nyengine (L2), bali pia wa utamaduni, mawazo na miundo tofauti ya lugha.

Munday (2007) anasema tafsiri kama dhana ina maana pana, ambayo upande mmoja inakusudia kazi iliyotafsiriwa na kwa upande mwengine mchakato, yaani kitendo cha kutafsiri. Mchakato wa tafsiri kati ya lugha mbili tofauti unajumuisha kazi ya mfasiri kubadilisha matinzi chanzi iliyo kwenye lugha ya asili (L1) kuwa matini lengwa katika lugha nyengine (L2), ingawa pia kwa mujibu wa Munday inaweza kuwa kwenye mfumo wa matamshi au alama nyengine za kimawasiliano na sio lazima iwe maandishi tu. Hata hivyo, mawazo haya ya Munday, yanachanganya kuhusu dhana ya

tafsiri na ukalimani. Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu tafsiri inahusisha matini andishi kama ambavyo imeelezwa na wataalamu wa tafsiri(Catford,1965; Newmark, 1988 na 2003; Mwansoko,1996; Nord, 2006) hawa ni baadhi tu.

Kwa upande mwingine, fasili ya Munday inatokana na dhana ya "utatu wa fasili ya tafsiri" ambao ni:

(i) *Tafsiri ya ndani ya lugha moja* inayofasiri kazi ya lugha hiyo hiyo kwa kutumia maneno mengine ya lugha hiyo hiyo;

(ii) *Tafsiri baina ya lugha tofauti* inayotafsiri maneno ya lugha moja kwenda lugha nyingine;

(iii) *Tafsiri ya kisimiotiki* inayotafsiri maneno ya lugha kuwa alama nyengine za mawasiliano, kama vile alama za barabarani au lugha ya watu wenye ulemavu wa kusikia au kuona au hata kutoka maneno kwenda kwenye ala za muziki na sauti.

Aidha, si lengo la utafiti huu kuzungumzia vipengele vyote vya utatu wa tafsiri, na hivyo mtafiti alijikita zaidi katika kuifasili tafsiri kwa kutumia (ii) hapo juu, yaani *tafsiri baina ya lugha tofauti* inayotafsiri maneno ya lugha moja kwenda lugha nyengine;

Akizungumzia suala la ujuzi wa lugha kwa mfasiri, Gouadec (2007) anaelezakuwa, licha ya kwamba kujua lugha zaidi ya moja ni jambo la muhimu katika tafsiri, lakini hakutoshi. Badala yake mfasiri anahitaji kuwa na weledi wa lugha na uelewa mpana wa utamaduni, historia, mitazamo, na mjengeko wa jamii ambazo lugha zake zinahusika kwenye kazi inayofasiriwa na pia weledi kwa mada yenyewe

inayofasiriwa. Suala la ujuzi wa lugha na sifa zingine zimejadiliwa kwa kina na Jilala (2014) katika kutumia Modeli yake ya M.M.K (Modeli ya Mawasiliano ya Kiutamaduni).

Jumuiya ya Wafasiri wa Taasisi za Elimu ya Juu nchini Marekani kama inavyonukuliwa na Samuelsson-Brown (2010) inataja sifa zifuatazo kwa mfasiri kukubalika kuwa mfasiri wa kweli:

(i) Anapaswa kuwa na hisia za lugha na mapenzi nayo.

(ii) Anapaswa kuwa na uwelewa mkubwa wa lugha chanzi na utamaduni na fasihi ya eneo inakotoka lugha hiyo na pia ufahamu wa kutosha wa mada anayoitafsiri.

(iii) Awe anazijua kazi nyingine za mwandishi wa kazi anayotafsiri.

(iv) Awe mwandishi mbunifu wa lugha lengwa inayokaribiana na kuwa mzawa wa lugha hiyo.

(v) Awe na uwezo wa kuhama kutoka muundo mmoja wa lugha kwenda mwengine anapofasiri kazi tofauti.

(vi) Awe na dhamira ya kutoa maana ya kazi ya asili.

(vii) Aweze kutoa matini inayosomeka vyema kwa kuakisi mwangwi wa lugha chanzi kama kwamba mwandishi mwenyewe alikuwa akiandika kwa lugha lengwa.

Kwa ufupi na kama inavyowekwa kitaalamu zaidi na Nchimbi (1976) kwenye makala yake Mwongozo wa Suala la Kutafsiri Nchini Tanzania: “Maadam tafsiri inamhitaji anayetafsiri kufahamu barabara habari yenyewe inayotarajiwa kutafsiriwa, yaani Ll na pia kuifahamu barabara miundo mbaIimbaIi ya lugha L2 ambamo tafsiri hiyo itafanyika, ni dhahiri kwamba, aina yoyote ya tafsiri lazima ifanyike katika lugha

ambayo anayetafsiri awe amezaliwa nayo. Zaidi ya hayo, mambo ambayo yanasaidia kuifanya tafsiri yoyote iwe sahihi zaidi ni elimu ya mfasiri katika utamaduni, siasa na mazingira ya nchi ambamo lugha zinazotumika katika tafsiri hiyo zimekomazwa."

Matokeo ya kazi inayofanywa na mfasiri mwenye sifa hizo ni kama yale yanayoorodheshwa na Banjar (2010):

(i) Uhakika na ukweli: tafsiri hutoa ujumbe uliokusudiwa bila kuongeza wala kupunguza maana.

(ii) Mantiki: tafsiri huzingatia mantiki iliyomo kwenye lugha lengwa.

(iii) Ufasaha: tafsiri husema kwa ufasaha na urahisi kinachotafsiriwa.

(iv) Ukawaida: tafsiri hutumia lugha ya kawaida na isiyochangaya.

(v) Utimilifu: tafsiri hutimiza lengo la matini chanzi.

(vi) Uzingatifu: tafsiri humzingatia mlengwa wa kazi inayotafsiriwa.

Hayo hutokezea kwa sababu, mfasiri husimama kama daraja linalomuunganisha mlengwa na mwandishi wa ujumbe katika lugha chanzi. Japokuwa lengo la utafiti huu halikuwa kuchunguza sifa za mfasiri, uelewa huu wa sifa za mfasiri na kile anachotakiwa kukijua ulitusaidia kuelewa na kubainisha changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata na jinsi mfasiri mwenye sifa anuai anaweza kuepuka changamoto hizo. Vilevile ilitusaidia kubaini changamoto za kutafsiri matini za Kiingereza kwenda Kiswahili na pia kuibua sababu za changamoto hizo.

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba kufasiri kulianza zamani sana hata kabla ya kuzaliwa Krisito. Sayansi na taaluma nyingi zilizoanza Misri kwenye miaka ya 3000 na zaidi kabla ya kuzaliwa Kristo zilitufikia sisi na mataifa ya Ulaya kwa njia ya

tafsiri (Mwansoko, 1996:4; Mshindo, 2010:18) kupitia kwa wataalamu wa Kiyonani. Wataalamu wa Ulaya walitafsiri kwa Kilatini vitabu kutoka kwenye Ulimwengu wa Kiisilamu vilivyokuwa vimetafsiriwa kwa Kiarabu kutoka kwa Wayonani na kuvipeleka kwao Ulaya na kuchota maarifa yaliyokuwamo ndani yake.

Kazi nyingi za kutafsiri ziliibuka katika karne ya 12 na kushika kasi katika karne ya 19 na 20. Katika karne iliyopita matini nyingi zilizotafsiriwa zilikuwa za kidini, fasihi, sayansi na falsafa (Mshindo 2010:18). Karne ya 20 inajulikana kama karne ya tafsiri kutokana na wingi wa tafsiri (Mwansoko 2006:4 inayoitwa Hamziya, ni utenzi wa Kiarabu uliotungwa kwenye karine ya kumi na tatu (amekwishatajwa), kwenye karne ya 19, wamisionari walitafsiri vitabu vingi vya Kikristo kwa Kiswahili na baadhi ya lugha za makabila makubwa ya Tanzania.

Wakati wa ukoloni maandiko mengi ya fasihi ya ulaya na Asia yalifasiriwa kwa Kiswahili mfano, Hekaya za Abunuasi na hadithi nyingine, *Alfulela ulela* au siku elfu na moja, Robinson Kruso na kisiwa chake n.k. Baada ya uhuru wazalendo walijaribu kufasiri vitabu bora vya ulimwengu kwa Kiswahili, kwa mfano, hayati baba wa Taifa Mwalimu J. Nyerere alitafsiri vitabu viwili vya tamthiliya vya William Shakespeare vya *Merchant of Venis* "Mabepari wa Venisi, na *Julius caisar* "Juliasi Kaisari", Paul Sozigwa naye alitafsiri kitabu cha ushairi cha Song *of Lawino* "Wimbo wa Lawino".

## 2.3 Tafiti kuhusu tafsiri

Zipo tafiti mbalimbali ambazo zilizofanywa kuhusu matatizo, changamoto za kutafsiri matini za kifasihi, matini za kiufundi na matini za kiutamaduni kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili na kinyume chake. Baadhi ya watafiti

hao ni Malangwa (2005 na 2010), Mtui (2009), Enea (2010) na Ngunguti (2010), na Jilala (2014).

Kwa mfano, Malangwa (2005) alichunguza juu ya changamoto za kutafsiri matini za kifasihi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kwa kutumia mfano wa mchezo wa kuigiza wa *Mabepari wa Venisi* iliyotafsiriwa na Mwalimu J.K. Nyerere. Katika utafiti wake alibaini kuwa wafasiri hupambana na changamoto za kimuundo na kiutamaduni kwa sababu lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili ni lugha zinazotofautiana kisarufi. Tofauti na utafiti wa Malangwa, utafiti huu ulijikita zaidi katika kuchunguza changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza. Aidha, utafiti wa Malangwa ulitusaidia katika kufanya majumuisho ya changamoto za kutafsiri matini za Kiswahili kwenda Kiingereza.

Kwa upande mwingine Bani (2006) katika utafiti wake anaeleza kuwa tafsiri ya kwenye vyombo vya habari ni matokeo ya kile alichokiita "ulazima wa uharaka", unaomaanisha kwamba lazima mfasiri afanye kazi ya kuhawilisha ujumbe kutoka lugha moja kwenda nyingine kwa kasi ambayo baada ya muda mchache awe ameshakamilisha kazi hiyo na kuiwasilisha kwa hadhira lengwa, ikiwa na maana iliyokusudiwa kwenye lugha chanzi. Uharaka huu unaathiri matokeo ya kazi ya tafsiri. Swali la kujiuliza hapa ni kwamba je, uharaka huo ndio unaweza kusababisha changamoto za kutafsiri sentensi tata?

Kwa upande mwingine, Malangwa (2010) alifanya utafiti kuhusu namna ya kuzikabili matini za kiufundi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kwa kutumia mifano ya programu za kompyuta. Katika utafiti huo, aligundua kuwa moja ya changamoto

wanazozipata wafasiri wanapotafsiri matini za kiufundi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili ni pamoja na tofauti za lugha, utamaduni na ukosefu wa visawe linganifu. Tofauti na utafiti wa Malangwa, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na wala si matini za kiufundi.

Naye Enea (2010) alifanya utafiti kuhusu changamoto za kutafsiri matini za habari za BBC zinazofanywa na waandishi wa habari wa TBC. Katika utafiti wake alihitimisha kuwa, lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili ni lugha zinazotafautiana katika muundo, muktadha, mazingira na utamaduni. Hivyo ni dhahiri kuwa kuna makosa ya kisarufi ambayo yanajitokeza katika matini za habari kutokana na tofauti za lugha hizo. Utafiti wa Enea ulikuwa chachu ya utafiti huu ambao ulichunguza changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka katika Kiswahili kwenda Kiingereza.

Kwa mujibu wa utafiti huo, kwanza kuna makosa yanayofanyika katika ufasiri kwenye vyombo vya habari vya Kenya na pili, makosa hayo yanatokana na athari za lugha ya kwanza ya mwandishi ambayo ama si Kiswahili wala si ile lugha ya kigeni kama Kiingereza na pia kiwango duni cha ujuzi wa msamiati. Utafiti huu unachunguza changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ili kuona ni jinsi gani tunaweza kukabiliana na changamoto hizo katika kuleta ufanisi wa mawasiliano.

Jilala (2014) alichunguza athari za kiutamaduni katika tafsiri ya matini za kitalii katika makumbusho ya Tanzania, lengo lilikuwa ni kuunda Modelikwa ajili ya ufanisi wa mawasiliano. Tofauti na utafiti wa Jilala, utafiti huu unachunguza changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata na athari zake katika ufanisi wa mawasiliano.

## 2.4 Dhana ya Utata, Fasili na Chanzo Chake

Utata katika sentensini hali ambapo sentensi moja huwa na maana zaidi ya moja au huweza kueleweka kwa namna zaidi ya moja. Kwa upande wa aina za utata tunaweza kupata aina zifuatazo:

(i) Utata wa kilesika: huu ni utata ambao husababishwa na neno au maneno fulaniyaliyotumika katika sentensi ambayo yana maana zaidi ya moja. Kwa kawaida utata wa kileksika hutokana na matumizi ya uhonimia na upolisemia, kwa mfano; a) Baada ya shida nyingi alifanikiwa kumleta papa nyumbani. Hii inaweza kuwa na maana mbili, mosi, aina ya samaki na pili kiongoziwa kanisa katoliki

(ii) Utata wa Kimuundo, huu hutokana na jinsi sentesi zilivyopangiliwa na kutokana na umbo, kirai au neno kuwa katika nafasi maalumu katika sentesi. Kwa mfano: tazama sentensi hii“Wanaume na wanawake waangalifu walikaa kando” sentensi hii ina maana ya: i) wanaume walikaa kando na wanawake waangalifu walikaa kando, ii) Wanawake waangalifu walikaa kando na pia wanume waangalifu walikaa kando.

Katika kuelezea sababu zautata katika sentensi, Taasisi ya Elimu (1994) wameelezea sababu zinazochangia kutokeakwa utata katika sentensi kama ifuatavyo:

(i) Neno kuwa na fahiwa zaidi ya moja, kwa mfano neno mbuzi, kata n.k.

(ii) Kutozingatia taratibu za uandishi, Mfano; Tulimkuta Nyammy na rafiki yake, Mazala vsTulimkuta Nyammy rafiki yake Mazala. Katika sentensi hizi alama (,) ndio huleta tofauti, sentensi ya kwanza inamaana kulikuwa na watu wawili Nyammy na rafiki yake aitwaye Mazala na sentensi ya pili isiyo na alama (,)

inamaanisha kulikuwa na watu wawili Nyammy na mtu mwingine ambaye ni rafiki yake Mazala.

(iii) Kutumia maneno bila kuzingatia muktadha wa matumizi ya maneno hayo.

(iv) Utamkaji wa maneno

(v) Mjengo wa maneno

Utata huu huzuka katika vitenzi kama pigia. Chanzo cha utata katika kitenzi hiki ni –i- inaweza kumaanisha: kwa ajili ya…, kwa sababu ya.., kwa kutumia chombo fulani.., au mahali fulani.  Kwa mfano:

(i) Alimpigia ukorofi wake (kwa sababu ya)

(ii) Alimpigia kiatu (kifaa)

(iii) Alimpigia ndani (mahali)

Aidha Taasisi ya Elimu wamebainishambinu za kuondoa utata katika tungo kama zifuatazo:

Kwanza, kutoa ufafanuzi kwa maneno ambayo yana maana zaidi ya moja na kuongeza viambishi ili kubainisha maana iliyokusudiwa.

Pili kuzingatia kanuni za uandishi, mwandishi akizingatia alama za uakifishi kwa kuweka alama sehemu husika ili iweze kueleweka na msomaji. Vilevile kuzingatia matumizi sahihi katika mazingira sahihi ya viunganishi na vihusishi.

Tatu, kumbuka kuweka shada mahali inapohitajika au kuitofautisha kwa kuweka hati mlazo ili kuitofautisha na maneno mengine. Vilevile mwandishi atumie visawe faafu katika tungo ambavyo havitakuwa na maana zaidi ya moja.

Nne, kuepuka matumizi ya lugha ya kifasihi mahali pasipohitajika. Lugha hiyo itumike katika mazingira na wakati unaofaa. Mfano unawaandikia watoto badala ya kuandika amevaa miwani itumike amelewa ili iweze kueleweka kwa urahisi.

**Tafiti kuhusu Utata katika Lugha**

Petre (2012) alifanya utafiti ambao ulieleza lugha yeyote ni tata.Pia akasema kuwa utata katika lugha unaifanya lugha kuwa madhubuti zaidi kwa sababu inahusu matamshi sahihi na mafupi ambapo msikilizaji anaweza kutofautisha kwa urahisi.Lakini pia akasisitiza kuwa utapoielewa ile lugha vizuri basi anasema utata katika lugha si tatizo.

Kotokana na utafiti huo ambao unaoneshea faida za utata katika lugha kwa jumla ndio uliomsababisha mtafiti kutaka kutafiti changamoto za kutafsiri sentensi za Kiswahili sanifu zenye utata kwenda Kiingereza mada ambayo Petre hajaweza kuzungumzia kwani yeye amezungumzia faida za utata katika lugha kwa jumla ingawa aligusia kuwa lugha yoyote ni tata.

Naye Solomon (2014)anasematungo tata ni zile ambazo huwa na maana zaidi ya moja. Anaendelea kusema kuwa, utata hujitokeza zaidi kwenye maandishi kuliko katika lugha ya mazungumzo. Mwandishi kaonesha kuwepo kwa sababu kadhaa zinazosababisha utata katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa sababu hizi ni pamoja na neno kuwa na maana zaidi ya moja, kutozingatia taratibu za maandishi, kukosekana kwa shada au mkazo, matumizi ya fasihi n.k.Mwandishi wamakala hii pia kaonesha mbinu mbalimbali za kuondoa utata ambazo ni pamoja na, kuzingatia kanuni za uandishi, kuweka shada, kuepuka matumizi ya lugha ya kifasihi n.k.

Makala hii imeeleza tu kwa ufupi sababu na mbinu za kuondoa utata.Haikujihusisha kabisa na changamoto za tafsiri ya tungo tata kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.Hivyo, mtafiti katika kuyakamilisha malengo yake aliendelea kufanya marejeo ya kazi nyengine mbalimbali.

Aidha, Bakari (2014), akimnukuu Traole (2005) ameandika kuhusu tafsiri ya kitabu cha *Utengano* kutoka lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiitaliano. Amejaribu kuonesha matatizo yaliyomo katika kutafsiri mbinu za kimtindo kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiitaliano. Pamoja na kwamba kazi hii imezingatia tafsiri ya kitabu kizima kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine, lakini mwandishi wake amejikita zaidi katika mbinu za kimtindo na hivyo hakuonesha changamoto zozote zinazojitokeza katika kutafsiri sentensi za Kiswahili sanifu kwenda katika lugha ya Kiingereza. Hivyo mtafiti ameonesha changamoto hizo kwa namna ya malengo yake alivyojiwekea.

Mwangi (2016) amejadili changamoto mbali mbali ambazo husababishamatatizo katika kutafsiri lugha moja kwenda lugha nyengine. Anafafanua kwa kusema kwamba kila jamii ina utamaduni wake ili kuelewa lugha fulani na dhana zinazohusishwa na hiyo lugha, itabidi awe mzawa wa utamaduni husika ama awe na tajriba ya utamaduni huo,hivyo utamaduni ni changamoto katika shughuli ya kutafsiri.Amejaribu kutoa changamoto hizo kupitia aina za vyakula vya kitamaduni katika jamii yaWamasai,mavazi na mapambo n.k.

Mwandishi kazungumzia zaidi kuhusu changamoto za utamaduni kuhusu lugha mama kwenda lugha ya Kiswahili kwa mintarafu hiyo hakujihusisha na lengo la

mtafiti.Hivyo utafiti huu ulifanyika kwa lengo la kuziba pengo ambalo linajidhihirisha katika utafiti huu.

Chakata (2013)inajaribu kuangalia suala la utata unaojitokeza katika tungo za Kiswahili.Mwandishi amejielekeza zaidi katika tungo virai vya lugha ya Kiswahili.Mwandishi anaeleza kwamba,miongoni mwa wanafunzi wanaosoma katika kozi ya Isimu hukabiliwa na utata katika dhana ya uainishaji wa virai, aidha baadhi ya mifano inayotolewa katika kushadidia aina za virai inakinzana na virejelezi vinavyotangulia.

Suala hili sio tu linawachanganya wanafunzi bali pia walimu wanaotarajiwa kuwaelekeza wanafunzi mashuleni. Makala hii inachunguza kwa kina maana ya virai,mifano ya virai na kupendekeza mbinu mwafaka za kuondoa utata katika virai. Mwandishi wa Makala hii anajikita zaidi katika suala la utata hasa katika virai na hakujihusisha na suala la changamoto za kutafsiri tungo tata za Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza. Hivyo mtafiti ana kila sababu ya kuendelea na kazi yake ili kukamilisha malengo yake.

Jenga (2014), alifanya utafiti kuhusu changamoto za tasnia za kutafsiri matini za kisheria kama zilivyo katika sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya.Katika kazi yake hii ameeleza kwa upana dhana ya tafsiri kisheria pamoja na dhima yake.Ameendelea kwa kuainisha matini za kisheria, sifa za jumla za matini hizo na mwisho amemalizia na changamoto za kutafsiri matini za kisheria.Mwandishi hakujihusisha na changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata za Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza.

Said (2015) ameandika tasnifu yake kuhusu Tofauti Za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi Baina ya Wazungumzaji wa Kiswahili. Said amejikita zaidi katika lahaja za Kipemba na jinsi mawasilianno yanavyokwamishwa, hakuzungumzia kabisa katika masuala ya athari na changamoto za tungo zenye utata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

Baada ya kupitia machapisho mbali mbali kuhusiana na mada ya mtafiti, imedhihirika kuwa kumefanyika tafiti chache sanakuhusu utata katika sentensi. Hakuna utafiti wowote uliofanywa na unaolingana moja kwa moja na mada ya mtafiti. Aidha ni machapisho machache yaliyojitokeza kujadili suala la athari za tungo zenye utata za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda lugha ya Kingereza. Hivyo ni wazi kwamba mada hii haijafanyiwa utafiti wa kutosha na ndio maana mtafiti alidhamiria kufanya utafiti huu.

## 2.5 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu ulitumia nadharia ya Ulinganifu wa kimuundo ambayo inasisitiza ulinganifu wa kimuundo baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Kipengele kinachofuata kitaelezea kwa kina nadharia ya ulinganifu wa kimuundo.

### 2.5.1 Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo

Huu ni mkabala wa kimapokeo katika tafsiri unaosisitiza tafsiri ya neno kwa neno au tafsiri sisisi ya matini. Catford (1965) anaeleza, moja kati ya kazi ya nadharia ya tafsiri ni kufasili matini asilia kwa kutumia hali na ulinganifu katika tafsiri. Ulinganifu anaoutaja katika nadharia yake ya Ulinganifu wa Kimuundo unahusishwa na msingi ambao nafasi ya matini chanzi inachukuliwa na matini lengwa. Hii ina maana kwamba

katika zoezi la tafsiri mfasiri hushughulika na ubadilishaji wa maana, maumbo ya kiisimu ya lugha chanzi na yale ya lugha lengwa na siyo uhamishaji wa mambo hayo. Kwa mfano, katika tafsiri ya aina hii, kirai nomino cha lugha chanzi kinabadilishwa kwa kutumia kirai nomino cha lugha lengwa.

Makaryk (1993) anaeleza kuwa, kwa kutumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo, mfasiri hujaribu kubadilisha maneno na muundo wa kisarufi wa lugha chanzi kwenda kwenye maneno na muundo wa kisarufi unaofanana nao katika lugha lengwa, bila kujali athari itakayojitokeza, kama vile lugha lengwa kutokueleweka na kukosa uasilia (taz. Pym, 2010).

Katika Nadharia hii, Catford anaiona lugha kama seti ya mfumo unaofanya kazi katika viwango tofauti. Mtazamo huu unampa uhuru wa kufasiri na kuweka ulinganifu wa matini katika vigezo vya aina tatu. Kigezo cha kwanza kimejikita katika masuala ya kisarufi ama ya kifonolojia ambayo ndiyo chimbuko la kuibuka kwa ulinganifu. Kwa kutumia kigezo hiki Catford anatofautisha kati ya tafsiri ya safu ukomo na tafsiri ya safu isiyo ukomo. Kigezo cha pili kimejikita katika viwango vya lugha vilivyohusishwa katika tafsiri ambapo tofauti inajengwa kati ya tafsiri pana na tafsiri finyu. Katika tafsiri pana, vipengele vyote vya matini ya lugha chanzi huchukuliwa na vipengele vya lugha lengwa. Hii ina maana kwamba, ulinganifu katika tafsiri ya aina hii hujikita katika sarufi na msamiati wa lugha. Catford (1965: 22) anafasili tafsiri pana kama uhamishaji wa sarufi ya lugha chanzi na msamiati wake kwa kutumia visawe vya sarufi ya lugha lengwa na msamiati wake. Kwa upande mwingine, tafsiri finyu ni ile inayohusisha uhamishaji wa vipengele vya matini ya lugha chanzi na visawe vyake kwa kutumia vipengele vya lugha lengwa.

Kigezo cha mwisho ambacho Catford anakisisitiza katika uhamishaji wa matini kimejikita katika kiwango cha tafsiri ambapo anatofautisha kati ya tafsiri kamili na tafsiri isiyo kamili. Katika tafsiri kamili, mchakato wa kutafsiri matini yote inabadilishwa kutoka katika lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa.

Katika tafsiri isiyo kamili, baadhi ya sehemu za matini ya lugha chanzi hutafsiriwa na nyingine hubaki bila kutafsiriwa. Hii ina maana kwamba, wakati wa mchakato wa uhawilishaji wa matini chanzi baadhi ya vipengele vya matini ya lugha chanzi huhamishwa kwa kutumia vipengele vya matini ya lugha lengwa na wakati huohuo kuna baadhi ya vipengele katika matini chanzi huachwa bila kutafsiriwa. Mkabala huu, unaitazama tafsiri kama njia ya kubadili kila kipengele cha lugha chanzi kwa kutumia visawe vya lugha lengwa.

Mkabala huu unapingwa na baadhi ya wataalamu wa tafsiri. Kwa mfano, Baker (1999) kama alivyonukuliwa na Malangwa (2010:46) anapinga mawazo ya Catford. Anaona kuwa, Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo haiendi mbali zaidi ya kutumia sentensi ili kuunganisha matini kama kiungo cha maana. Anaendelea kusema kuwa, nadharia hii haina uasilia unaoweza kutoa maelezo sahihi ya tafsiri kutoka katika mtazamo wa kiisimu. Tafsiri ya ulinganifu wa kimuundo husababisha uzalishaji wa matini ya lugha lengwa ambayo ni muunganiko wa maneno ya lugha lengwa, sintaksia ya lugha lengwa na ile ya lugha chanzi (Malangwa, 2010). Nadharia hii inapotumika huweza kuifanya tafsiri (matini lengwa) kuwa ngumu zaidi kusomeka na kueleweka kuliko ilivyo matini chanzi. Aidha, baadhi ya miundo ya lugha chanzi inaweza isieleweke katika lugha lengwa kwa sababu miundo na maumbo ya maneno katika lugha hutofautiana kutoka lugha moja na lugha nyingine. Kila lugha ina sarufi yake;

hivyo basi kwa kutumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo tunaweza kusababisha tatizo la mawasiliano.

Utafiti huu utatumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo katika kuchunguza za kuchambua data za utafiti huu. Nadharia hii ilionekana inafaa katika kutimiza malengo ya utafiti huukwa kuwa inaweza kubainisha changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata.

## 2.6 Muhutasari

Sura hii ya pili imechambua kwa kina mapitio ya kazi tangulizi za kinadharia na kiutafiti.Pia imeeleza kiunzi cha Nadharia ambapo tumefafanua Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo ambayo itatuongoza katika kufikia malengo ya utafiti huu. Katika sehemu inayofuata tutaelezea mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utaftiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili mikabala, mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Kwa ujumla utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya, kuzichambua, kuziwasilisha na kuzijadili data za utafiti huu. Kwa hiyo, utafiti huu ulihusisha nduni za utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika misingi ya ukamilishano na ujazilizano. Kwa ujumla, sura hii inajadili yafuatayo: eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, utafiti tangulizi, mbinu za ukusanyaji data, uthabiti na kuaminika kwa uchambuzi wa data na hitimisho.


## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti huu katika sehemu kubwa ni wa maelezo. Usanifu wa maelezo kama ulivyofafanuliwa na Cohen (2007) ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Mtafiti huzipanga kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Mtafiti amekuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, kuvunbua, kufanya majaribio, kutafisri tarifa alizozozipata kupitia mundo huu wa utafiti. Sehemu ndogo ya utafiti imetumia takwimu kama kielezo.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika wilaya za Magharibi A&B na Wilaya ya mjini. Utafiti huu umefanyika Chuo Kikuu cha Chukwani, Shule ya Sekondari ya Kwerekwe C, Shule ya Al-hisan na Shule ya S.O.S ambazo ziko Wilaya ya Magharibi A. Pia umefanyika Chuo Kikuu cha SUZA kilichopo Wilaya ya

Magharibi B. Katika Wilaya ya Mjini utafiti umefanyika katika shule msingi za Faraja, vikokotoni na Kiponda. Pia katika Wilaya ya Mjini wanapatikana waandishi wa habari, wakalimani na wafasiri mbalimbali ambao ni miongoni mwa watafitiwa.Uteuzi wa sehemu hizi umezingatia kwamba watafitiwa ni walimu, wanafunzi na wafasiri. Kwa hiyo ilikuwarahisi kupata data ambazo ni halisi kutoka kwa watafitiwa waliokusudiwa.




**Kielelezo Na. 3.1: Ramani ya Sehemu Zilizofanyiwa Utafiti**

Chanzo: mtandao wa Google Mei, 2017

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni istilahi inayotumiwa katika masuala ya utafiti kurejelea watafitiwa wachache kutoka kundi lengwa ambalo huteuliwa na mtafiti ili watumike kutoa taarifa zinazochunguzwa na mtafiti (Kothari, 2004). Cooper (1989) anaeleza kuwa kundi lengwa katika utafiti linahusisha jamii nzima, makundi ya watu, au vitu vingine ambavyo kwavyo mtafiti atavihusisha kama chanzo cha data.

Enon (1998) anaendelea kudai kuwa kundi lengwa ni vitu au watu ambao mtafiti anatarajia kupata au amepata data za utafiti wake. Kwa hivyo, mtafiti amefanya uchunguzi wa kuonyesha changamoto za kutafusiri sentensi za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza katika makundi mbalimbali ya jamii yanayoishi katika Mkoa wa Mjini magharibi.

Usampulishaji kwa mujibu wa Kothari (2004) ni mchakato wa kuteua sampuli ya watafitiwa wachache kutoka katika sampuli kuu zitakazotumika katika utafiti kuwakilisha wango nzima. Utafiti huu umeteua sampuli ya watafitiwa wachache kutoka wilaya tatu za Mkoa wa Mjini Magharibi kuwakilisha idadi kubwa ya jamii.

#### 3.4.1 Sampuli ya Watafitiwa

Kiutafiti, sampuli ya watafitiwa hutakiwa ijitosheleze na iwe ni ile inayotokana na kile mtafiti anachotaka kukitafiti. Pia, ni sampuli inayowakilisha eneo msingi la utafiti. Kwa hiyo, kutokana na maelezo ya hapo juu, sampuli ya utafiti huu imehusisha watafitiwa 100. Mtafiti ameamua kutumia idadi hii ya watafitiwa 100ambayo aliona inatosheleza kutoa taarifa zinazotakiwa kwa utafiti huu. Mchanganuo wa watafitiwa hawaumeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na 3.1**: **Sampuli ya Watafitiwa Katika Maeneo Teule**

| Na. | Watafitiwa | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Walimu wa somo la Kiswahili shule za sekondari | 15 |
| 2 | Wanafunzi wa shule za sekondari | 20 |
| 3 | Wanafunzi wa Kiswahili vyuo vikuu vya SUZA na Chukwani | 50 |
| 4 | Wahadhiri wa Kiswahili chuo Kikuu SUZA | 5 |
| 5 | Wafasiri | 10 |
| | **JUMLA** | **100** |

Chanzo utafiti wa uwandani 2017

Mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi kupata idadi ya watafitiwa inayotakiwa. Usampulishaji nasibu tabakishi ni mbinu inayoangalia makundi madogo madogo yaliyomo ndani ya kundi kubwa na sampuli huchaguliwa kinasibu kutoka kundi hilo (Kothari, 2004). Sampuli inayoteuliwa huwa na nafasi sawa ya kuweza kuchaguliwa kutoka katika idadi kubwa ya watu. Kwa kutumia usampulishaji nasibu tabakishi, jumla ya watafitiwa 100 walipatikana na miongoni mwao 50 walikuwa wanawake na 50 wanaume. Sababu za kugawanya sampuli ya watafitiwa katika makundi hayo ya wanaume na wanawake ilikuwa kutaka kupata mtazamo tofauti kulinganana jinsia.

Ili kupata taarifa za watafitiwa kutoka katika makundi mengine ya kijamii, suala la umri, kazi na elimu lilizingatiwa ambapo kulikuwa na sampuli ya watafitiwa mchanganyiko, yaani wazee wa kuanzia miaka 56 na zaidi, kundi la *umri wa kati kuanzia 36-55 na vijana wenye umri kati ya miaka 16-35.* Sababu ya kuzingatia makundi haya mchanganyiko ilikuwa kutaka kuchunguza na kuelewa uelewa wa kundi hili kuhusu changamoto hizo.

Kundi la walimu na wanafunzi wa shule za sekondari limetumiwa na mtafiti kupata majibu ya swali la kwanza na la pili la utafiti huu. Walimu na wanafunzi wamemsaidia mtafiti kupata majibu juu ya swali kuhusu;

(i) Aina za tungo zenye utata katika lugha ya Kiswahili sanifu zenye changamoto ya kutafsiri kwenda Kiingereza.

(ii) Changamoto zilizopo katika kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na madhara yake katika mawasiliano yenye ufanisi baina ya wazungumzaji wa lugha hizo.

Pia amewatumia wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu vya SUZA na Chukwani wa somo la Kiswahili kupata majibu ya maswali kuhusu:

(a) Changamoto zilizopo katika kutafsiri tungo za lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na madhara yake katika mawasiliano fanisi ya wazungumzaji wa lugha hizo mbili.

(b) Athari za tungo za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda lugha ya Kiingereza katika mwasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha hizo.

Vilevile amewatumia wahadhiri na wafasiri kupata changamoto na athari zilizopo katika kutafsi tungo tata kutoka lugha ya Kiswahili sanifu kwenda lugha ya Kiingereza. Sababu za kutumia makundi haya katika ukusanyaji wa data ni kuweza kupata taarifa za kiutaalamu zinazohusu mada hii. Hii imetokana na kuwa utata hujitokeza kwa kiasi kikubwa katika mazungumzo kuliko maandishi.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data

Katika kuchunguza changamoto za kutafsiri sentensi za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza mtafiti ametumia mbinu mchanganyiko. Mbinu hizo ni hojaji, mahojiano

na maktaba. Lengo la kutumia mbinu hizi mchanganyiko ni kuthibitisha uhakika wa taarifa zilizotolewa na watafitiwa walioteuliwa katika utafiti huu.

### 3.5.1 Maktaba

Hii ni mbinu ambayo ina husu uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo Kothari (2004). Mtafiti alichagua mbinu hii kwasababu ilimuwezesha kupata taarifa za awali ambazo ndizo za msingi zitakazomsaidia katika kukamilisha malengo aliyojiwekea kupitia vitabu mbalimbali vya sarufi. Kwa kutumia njia hii mtafiti alipata data za uhakika zinazohusu changamoto za kutafsiri sentensi za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza.

### 3.5.2 Hojaji

Mbinu ya hojaji huhusisha orodha ya maswali na maelekezo ya jinsi ya kujibu maswali yaliyoandaliwa na mtafiti ili watafitiwa waweze kujibu maswali hayo (Kothari, 2004). Kuna hojaji funge na isofunge. Hojaji funge ina maswali ambayo humtaka mtafitiwa kuteua jibu kati ya majibu mengi na hojaji isofunge ina maswali yanayohitaji maelezo kutoka kwa mtafitiwa. Mtafiti ametumia hojaji yenye maswali funge na yasofunge kwa sababu mtafitiwa aliweza kutoa maoni yake kwa kujiamini zaidi katika kujibu maswali aliyoulizwa. Njia hii inaokoa muda katika kukusanya data na kuzichambua. Pia, haina gharama kubwa na hutunza siri za watafitiwa. Mtafiti ametumia hojaji ambazo zilimsaidia kupata taarifa zilizohusu watafitiwa, kupata taarifa za kiisimujamii na pia kupata changamoto za kutafsiri sentesi za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza.

Sababu nyingine ya kutumia mbinu ya hojaji ni kwamba ni njia ambayo ilimruhusu mtafitiwa kujibu maswali aliyoulizwa kwa namna anavyoelewa na kwa ufafanuzi wa kutosha. Pia, humjengea mtafitiwa hali ya kujiamini zaidi katika kujibu maswali aliyoulizwa. Hojaji inahusu maswali mbalimbali yanayolenga kupata taarifa sahihi za kubainisha changamoto za kutafsiri sentensi za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza. Mtafiti ametumia mbinu ya hojaji kutafuta taarifa zinazohusu;

(a) Aina za tungo zenye utata katika lugha ya Kiswahili zenye changamoto ya kutafsiri kwenda lugha ya Kiingereza na

(b) Athari za tungo zenye utata za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda lugha ya Kiingereza katika mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha hizo..

Mbinu ya hojaji imemsaidia mtafiti kupata taarifa kwa sababu watafitiwa wengi hawakuwa na nafasi ya mahojiano na kusababisha kuwapa hojaji ili waweze kuzijaza na kuzifuata siku nyingine. Pia mtafitiwa alipata muda wa kutosha wa kupitia maswali ya hojaji na kuyajibu kwa umakini.

### 3.5.3 Mahojiano

Kwa mujibu wa Enon (1998), mahojiano ni mbinu ya ukusanyaji wa taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya mdomo au majadiliano. Kuna aina tatu za mahojiano ambazo ni mahojiano funge, mahojiano huru na mahojiano nusufunge. Mahojiano funge ni mahojiano ambayo humhitaji mtafitiwa kujibu maswali yale tu yaliyoandaliwa na mtafiti. Mahojiano huru hutoa uhuru kwa mtafitiwa kuuliza au kujibu swali lolote kulingana na mahali na kitu chochote anachotaka kujua kwa wakati huo. Mahojianonusufunge humtaka mtafiti kuuliza maswali kadhaa yaliyofungwa na wakati huohuo anakuwa anafuatilia kwa undani jibu lililotolewa kwa

kutumia maswali yaliyo wazi. Utafiti huu ulitumia mbinu ya mahojiano na sababu ya kutumia mbinu hii ni:

Mtafiti ametumia mahojiano funge kutafuta taarifa juu ya maswali yafuatayo:

(a) Changamoto zilizopokatika kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na madhara yake katika mawasiliano yenye ufanisi baina ya wazungumzaji wa lugha hizo,

(b) Athari za tungo zenye utata za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda lugha ya Kiingereza katika mawasiliano yenyeufanisi baina ya wazungumzaji wa lugha hizo.

Katika kutumia mahojiano funge, kutafuta taarifa hizo, mtafiti amewahoji wahadhiri na wanachuo wa chuo kikuu cha SUZA, Chukwani na wafasiri.Mtafiti amewahoji wahadhiri na wanachuo wa SUZA na Chukwani kwa lengo la kupata data sahihi kwavile wao ndio wataalamu wa lugha ya Kiswahili. Pia wanauelewa wa kutosha kuhusu mada hii ya changamoto za kutafsiri tungo tatakutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

Mtafiti amewatumia wafasiri kwa sababu wanaelewa changamoto za kutafsiri tungo tata za Kiswahili kwenda Kiingereza kwani hufanya kazi ya kufasiri makala na vitabu vya Kiswahili kwenda Kiingereza na kinyume chake.

Mtafiti ametumia mahojiano huru kwa sababu yamempa mtafiti fursa ya kumdadisi zaidi mtafitwa. Kwa mujibu wa Kothari (1993), mahojiano huru humruhusu mtafiti kurekebisha maswali yake pale inapobidi. Mahojiano huruyalileta manufaa sana

katika utafiti huu kwasababu yametumika majadiliano ya ana kwa ana na mtafitiwa, kurekebisha baadhi ya maswali ya mahojiano kulingana na hali halisi iliyokuwepo, na kuibua baadhi ya maswali thakili baina ya wahojiwa mbalimbali.

### 3.6 Mbinu za Uchambuzi wa Data na Uwasilishwaji wa Matokeo

Data zilizopatikana katika utafiti huu zimechambuliwa kwa mkabala wa kiidadi na ule usio wa kiidadi.Mtafiti amechambua changamoto za kutafsiri tungo tata kwenda Kiingereza au kinyume chake kwa kuzingatia lengomoja baada ya jingine na mwisho ameeleza majumuisho yaliyogunduliwakatika utafiti wake.

Kwa upande wa uwasilishaji, data zimefafanuliwa kwa kutumia njia za kimaelezo. Njia ya kimaelezo ni ile inayotumika kufafanua jinsi watu wanavyofikiria na kuhisi kuhusu kitu au jambo fulani (Kothari, 2004). Njia ya kimaelezo imetumika kuelezea changamoto za kutafsiri sentensi za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza.

### 3.7 Muhtasari

Katika sura hii mtafiti ameeleza kuwa utafiti huu umefanyika katika wilaya za Mkoa wa Mjini Magharibi. Maeneo yaliyotumika katika ukusanyaji wa data ni shule za sekondari, vyuo vikuu na wafasiri.  Pia utafiti huu umetumia sampuli ya watafitiwa 100na mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi. Mtafiti ameeleza mbinu zilizotumika katika ukusanyanji wa data ni hojaji, mahojiano na maktaba. Njia zilizotumika kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa data za utafiti huu ni njia za kimaelezo na kitakwimu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI WA MATOKEO NA MAJADILIANO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data kutoka katika vyanzo mbalimbali vya data zinazohusu utafiti huu. Matokeo haya yamezingatia majibu ya watafitiwa kuhusu mambo yaliyotafitiwa kwa njia ya maktaba, dodoso na mahojiano.Data zimechambuliwa kwa mbinu zote za uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika sura ya tatuya taarifa hii ya utafiti kwa kujibu maswali ya utafiti yaliyoko kwenye sura ya kwanza ya kazi hii.Katika kujibu maswali ya utafiti yaliyoko kwenye sura ya kwanza,data zinalinganishwa na kulinganuliwa na matokeo ya utafiti ya tafiti zingine zilizojadiliwa katika sura ya pili ya kazi hii.

Lengo la sura hii ni kuwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti yaliyopatikana uwandani kuhusu changamoto za kutafsiri tungo tata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Sura hii imegawanywa katika sehemu nne. Sehemu hizi zimezingatia data zilizopatikana kutokana na malengo mahsusi ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inawasilisha, kuchambua na kujadilidata zilizopatikana kutokana na lengo la kwanza la utafiti huu, sehemu ya pili ni lengo la pili na sehemu ya tatu inatoa mjadala wa lengo la tatu. Sehemu ya nne inatoa hitimisho la sura.

## 4.2 Tungo Tata katika Lugha ya Kiswahili

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha aina ya tungo tata katika Kiswahili na changamoto zake katika tafsiri. Ili kupata data za swali hili, mtafiti alitumia mbinu ya usomaji wa machapisho kwa kusoma vitabu, majarida na

tafiti mbalimbali ili kubaini tungo tata katika lugha ya kiswahili. Data zilizopatikana katika vitabu zilidhihirisha kuwa katika lugha ya Kiswahili utata upo wa aina mbili ambazo ni utata wa maneno na utata wa sentensi. Utata wa maneno hujitokeza pale neno linapokuwa na maana zaidi ya moja kutegemeana na matamshi na mazingira ya neno linalohusika. Kwa mfano neno ‘paa’ na‘paka’. Maneno haya yana maana zaidi ya moja kama ifuatavyo:

(1) Paa

(i) Sehemu ya juu ya nyumba

(ii) Mnyama anayefanana na mbuzi

(iii) Kitendo cha kwenda juuangani

Matumizi ya neno ‘paa’yanadhihirisha kuwepo kwa maana zaidi ya moja kama ambavyo inajidhihirisha katika namba (i) hadi (iii) hapo juu. Hivyo, msikilizaji huweza kupata utata wa maana ya neno hilo hasa pale linapotumika bila kudhihirisha muktadha wa matumizi ya neno hilo.

(2) Paka

(i) Mnyama

(ii)Kitendo cha kupaka rangi katika kitu

Matumizi ya neno ‘paka’ huweza kuleta maana zaidi ya moja kama ambavyo inajidhihirisha katika namba (i) hadi (ii) hapo juu. Hivyo, msikilizaji huweza kupata utata wa maana ya neno hilo hasa pale linapotumika bila kudhihirisha muktadha wa matumizi ya neno hilo.Kwa upande wa utata katika tungo, huu ni utata ambao hujitokeza paletungo inapotoa maana zaidi ya moja zikisimama peke yake. Kwa mfano:

(1) Kata mbili

Sentensi hii ina maana zaidi ya moja

(i) Kitendo cha kukata vitu

(ii) Kifaa kinachotumika katika kuchotea ama kunywea maji

Mfano huo unadhihirisha kuwa sentensi ina utata, hivyo ili kuelewa maana iliyokusudiwa na mzungumzaji ama mwandishi ni lazima msikilizaji ama masomaji azingatie muktadha wa matumizi ya sentensi hiyo.

(2) Mtoto anaendesha

Sentensi hii inaweza kutoa maana kuwa:

(i) Anaendesha chombo usafiri barabarani

(ii) Ana maradhi ya tumbo la kuharisha

Katika sentesi hiyo hapo juu msikilizaji anaweza kujiuliza maswali msemaji amekusudia ama anaendesha chombo cha chausafiri barabarani kama vile gari. Au amepata maradhii ya tumbo la kuharisha na kusababisha kuibuka kwa maana zaidi ya moja.

Utata katika lugha ya Kiswahili sanifu hujitokeza zaidi katika neno kuliko katika sentensi, hii inatokana na kuwa katika mazungumzo jamii hutumia zaidi ya mkato kuliko sentensi.

### 4.2.1 Sababu za Utata katika Sentensi za Kiswahili Sanifu

Aidha, katika usomaji wa machapisho, utafiti huu uliweza kubainisha sababu zautata katika tungo za Kiswahili. Sababu hizo ni kama ifuatavyo;

(i) Neno kuwa na maana zaidi ya moja kama mbuzi, kata, paa n.k.

(ii) Kutozingatia taratibu za uandishi, kwa mfano: Tulimkuta Asha na rafikiyake, Rajab.

(iii) Kutumia maneno bila kuzingatia muktadha au mazingira yanayohusika na matumizi ya maneno hayo. Kwa mfano: *Ali ametumwa na Kombo.*

(iv) Utumiaji wa Maneno yenye maana ya picha au maana iliyofichika, yaani viashiria husababisha utata. Kwa mfano: *Nina ua mnyumbani pangu.* Tunapata maana kuwa wigo, sehemu ya mmea, anatoa uhai wa watu na maana nyingine nibinti mzuri.

(v) Kuwepo kwa kauli ya mofimu ya kutendea. Kwa mfano: *Amempigia ngoma*. Katika sentensi hizo msomaji anaweza kupata maana zifuatazo (i) Amempigia ngoma amfurahishe (ii) Amempigia kwa niaba yake (iii) Amempigia kwa kutumia ngoma.

(vi) Matumizi ya vimilikishi –ake- na –ao-, kwa mfano*: Ali atajenga kibanda chake*. Katika sentensi hiyo tunapata maana zifuatazo (i) Kibanda cha Ali (ii) Kibanda cha mtu mwengine.

(vii) Matumizi ya mzizi –ingine- kwa mfano*: Kingine kimepatikana*, katika sentensi hiyo msikilizaji anaweza kupata maana zifuatazo: (i) –zaidi ya (ii) –badala ya.

(viii) Matumizi ya baadhi ya viunganishi, kwa mfano*: Nilikutana na Frank na watoto wake*. Katika sentensi hii msomajii anaweza kupata maana zifautazo: (i) Frank aliandamana na watoto wake (ii) Nilikutana na Frank kisha nikakutana na watoto wa mtu mwengine.

(ix) Matumizi ya baadhi ya vihusishi, kwa mfano: *Ali anapenda kusoma kuliko Asha*. Katika sentensi hii tunaweza kupata maana zifuatazo: (i) Ali anapenda

kusoma zaidi ya vile anavyo mpenda Asha. (ii) Ali anapenda kusoma zaidi ya anavyopenda Asha.

(x) Makosa ya kisarufi na kimantiki, kwa mfano: *Kaka yako amerudi kazini* hapa tunapata maanakama vile (i) Kaka amerudi kutoka kazini (ii) Kaka amekwenda tena kazini (iii) Kaka haendi kazini.

Data katika mfano namba i hadi xi hapo juu zinadhihirisha kuwa utata katika lugha ya Kiswahili sanifu unasababishwa na mambo tisa ambayo ni: neno kuwa na maana zaidi ya moja, kutozingatia taratibu za uandishi, kutumia neno bila kuzingatia mazingira au muktadha, makosa ya kisarufi na kimantiki, matumizi ya baadhi ya vihusishi, matumizi ya baadhi ya viunganishi, matumizi ya mzizi –ingine-, matumizi ya vimilikishi ake- na ao-,kuwepo kwa kiambishi nafsi kiambata –a na wa,kuwepo kwa kauli ya kutendea,utumiaji wa maneno ya picha au maana liyojificha.

Baada ya kupata data za utata katika lugha ya Kiswahili kwa mbinu ya maktabani, data hizo zilijazilizwa na data zilizokusanywa kwa njia ya hojaji ambapo wahojiwa walitakiwa kutaja sentensi/tungo zenye utata katika Kiswahili. Kwa kufanya hivyo tuliweza kupata data ya sentensi/tungo zenye utata katika lugha ya Kiswahili zipatazo 139 na kisha kuzichambua na kuzijadili katika utafiti huu (taz. kiambatisho namba1).Data hizi zilimwongoza mtafiti katika kubainisha utata katika tungo za Kiswahili. Ubainishaji wa tungo hizo ulifanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui ambapo data zote zenye maana na ama sifa zinazofanana ziliwekwa katika kundi moja. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

### 4.2.2 Kubainisha Utata katika Sentesi za Kiswahili Sanifu

Katika Kiswahili sanifu tunaweza kubainisha utata kutokana na sababu iliyochangia kujitokeza kwa utata katika eneo hilo. Ufafanuzi ufuatao umeonyesha utata unaojitokeza kutokana na sababu mbalimbali katika Kiswahili sanifu.

#### 4.2.2.1 Matumizi ya Maneno Yenye Maana Zaidi ya Moja

Data zifuatazo zinaonesha kuwa katika lugha ya Kiswahili sanifu kunajitokeza utata unaosababishwa na matumizi ya maneno yenye maana zaidi ya moja.

(i) Amepata jiko

(ii) AjeJumanne

(iii) Amefanikiwa kununua mbuzi

(iv) Wewe nipe kata

(v) Sungura ana paa

(vi) Tafadhali niletee taa

Mifano katika data namba i hadi vi hapo juu inadhihirisha nomino zenye utata. Sentesi (i) amepata jiko, utata uko kwenye neno jiko, na kunapata maana tatu ambazo ni kama zifuatazo:

(a) Kifaa cha kupikia

(b) Maana ya tatu ni mke

(c) Mahali pa kupikia

Katika sentensi (ii) aje Jumanne, neno Jumanne ndilo lenye utata na linatupatia maana mbili ambazo ni:

(a) Maana ya kwanza aje siku ya Jumanne

(b) Maana ya pili ni jina la mtu (yaani aje mtu anayeitwa Jumanne)

Sentensi ya (iii) amefanikiwa kununua mbuzi, katika sentensi hii utata unajitokeza katika neno mbuzi na kutoa maana mbili tofauti ambazo ni:

(a) Maana ya kwanza amenunua mbuzi mnyama

(b) Maana ya pili amenunua kifaa cha kukunia nazi

Katika sentesi ya (v) wewe nipe kata, neno lenye utata ni kata na linatoa maana zaidi ya moja kama ifuatavyo:

(a) Maana ya kwaza ni kata ya kubebea mzigo

(b) Kifaa chakuchoteamaji

Sentensi ya (vi) sungura ana paa katika sentesi hii neno paa linatupatia maana zifuatozo:

(a) Maana ya kwanza paa la nyumba

(b) Pia kwa maana yapaa mnyama

Katika sentensi (vii) tafadhali niletee taa, hapa neno taa linaweza kuwa na maana zifuatazo:

(a) Taa kwa maana kifaa cha kinachotumika kutoa mwanga

(b) Taa kwa maana aina ya samaki anayepatikana baharini

Data zimeonyesha kuwa neno linaweza kutoa maana zaidi ya moja kama sentensi hizo hapo juu na husababisha ukwamishaji wa mawasiliano miongoni mwa wanajami wanaozungumza Kiswahili sanifu.

#### 4.2.2.2 Mofimu ya Kauli ya Utendea

Data hizo hapo chini zinaendelea kuonyesha utata ambao umesababishwa na mofimu ya kauli ya utendea, inapotumika katika mazungumzo au maandishi katika Kiswahili

sanifu husababisha kutokea kwa utata na kusababishamaana zaidi ya moja kupatikana. Data zinaonesha kuwa katika sentesi (i-v) maneno yenye utata ni vitenzi ambavyo vinaonyesha kauli ya utendea na kusababisha kujitokeza kwa maana zaidi ya moja kama data zinavyodhihirisha hapo chini:

(a) Amempigia ngoma,

(b) Amelalia uji,

(c) Amemuandikia Asha barua,

(d) Juma amelalia mkaa,

(e) Mwanafunzi alimpakia Doto,

Sentesi (i) Amempigia ngoma, katika sentensi imebeba mofimu ya kauli ya kendea \i\ na kunatoa maana zifuatazo:

(a) Amepiga ngoma ile amfurahishe

(b) Amepiga ngoma kwa niaba yake

(c) Amempiga kwa sababu ya ngoma

(d) Amempiga kwa kutumia ngoma

Sentesi (ii) Asha amemuandikia Omar barua, kitenzi amemuandikia kinatoa maana mbili ambazo ni:

(a) Asha ameandika barua kwenda kwa Omar

(b) Asha ameandika barua kwa niaba ya Omar

Sentensi (iii) Faki alimpigia kiatu, kitenzi alimpigia kinatupatia maana mbili ambazo ni:

(a) Maana ya kwanza alitumia kiatu kumpiga

(b) Pili alimpigia kama sababu

Data hizo hapo juu zimeonyesha kuwa utata unaweza kujidhihirisha katika mofimu za utendea kama vile neno moja lenye maana zaidi ya moja katika vitenzi vya kauli ya kutendea.

#### 4.2.2.3 Kutozingatia Taratibu za Uandishi

Kutozingatia taratibu za uandishi kuna sababishakujitokeza kwa utata katika sentesi za Kiswahili sanifu kama inavyojidhihirisha hapo chini. Data zifuatazo zinaendelea kuonesha kuwa utata katika lugha ya Kiswahili sanifu unajitokeza kwa kutozingatia matumizi sahihi ya taratibu za uandishi. Mwandishi anashindwa kutumia vyema alama za uakifishi katika maandishi hivyo kupatikana zaidi ya moja.. Alama hizo ni kama nukta, mkato, kiulizo na nyenginezo kama zinavyodhihirishwa katika sentensi zifuatazo:

(i) Mwalimu amesoma. Mwalimu amesoma?

(ii) Anakula na kijiko

(iii) Anaenda mjini na basikeli

(iv) Ali anatoka na Juma

(v) Tulimkuta Ali na rafiki yake, Said.

(vi) Tulimkuta Ali na rafiki yaka Said.

(vii) Nimemsomesha Asha na ndugu yake, Amina.

(viii) Nimemsomesha Asha na ndugu yake Amina

Data zimeonesha kuwa sentensi (i)Mwalimu anasoma.Mwalimu amesoma, inatoa maana mbili kwani sentesi inatoa taarfa na pia inatoa swali kinachotofautisha ni alama ya uakifishi. Sentensi (ii, iii) Anakula na kijiko na Anaenda mjini na basikeli. Sentensi hizi zina utata uliosababishwa na uakifishaji katika tungo hizo. Hali hii

imesababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya viunganishi au vihusishi. Katika sentensi ya (v) Ali anatoka na Juma. Katika sentensi hii halioneshwi waziwazi jambo linalomuhusu nani katika tungo na kusababisha tungo kuwa na utata kutokana na kutoonyesha mtendwa au mtendwa. Katika sentnsi ya (vii, viii) katika sentensi (vii) Tulimkuta Ali na rafiki yake, Said. Sentensi hii ina maana tuliwakuta watu wawili Ali na rafiki wa Ali, Rafiki huyo anaitwa Said. Alama ya mkato baada ya neno yake huuonyesha kuwa taarifa imekamilika na neno (Said ni ufafanuzi tu wa rafiki yake). Sentensi ya pili, tulimkuta Ali na rafiki yake Said, sentensi hii ina maana kuwa tulimkuta Ali na mtu mwingineambaye ni rafiki wa Said. Katika sentensi (ix, x) utata umejitokeza kama ifuatavyo: Katika sentensi nilimsomesha Asha na ndugu yake, Amina, hii ina maana niliwasomesha watu wawili Asha na ndugu wa Asha aliyeitwa Amina. Pia katika sentensi Nilimsomesha Asha na ndugu yake Amina maana yake nilimsomesha Asha na mtu mwingine ambaye ni ndugu yake na Amina.

#### 4.2.2.4 Kutumia Neno Bila Kuzingatia Mazingira au Muktadha Unaohusika

Kutumia neno bila kuzingatia mazingira au muktadha unaohusika husababishakuibuka kwa maana zaidi ya moja. Data zifuatazo hapo chini zinaonyesha kuwa utata unaweza kusababishwa na matumizi ya neno bila kuzingatia mazingira au muktadha unaohusika ambapo msomaji kushindwa kutumia mazingira yaliyo sahihi kama mifano inavyodhihirisha hapo chini:

(i) John amesomeshwa na Raju.

(ii) Ali amepigwa na Juma

(iii) Kaka amefungwa na baba

(iv) Wanafunzi wametumwa na mwalimu.

(v) Waziri analindwa na askari.

Katika sentensi (i) mwandishinamsomaji wataelewana ikiwa wote wanawajua Jonh na Raju, na hali ya uwezekano wa yupi amemsomesha mwezake. Tunapata maana mbili, maana ya kwanza ni John amesomeshwa na Raju na maana ya pili inawezekana Raju amesomeshwa na John. Hali hiyo imeendelea kujitokeza katika sentensi (ii) ambapo matumizi ya kiunganishi yamesababishakujitokeza kwa utata na kupatikana maana mbili.

**4.2.2.5 Kuwepo kwa Kiambishi Kiwakilishi Nafsi Kiambata (–a, –wa-)**

Data zinaendelea kubainisha kuwa utata katika Kiswahili Sanifu piaunasababishwa na kuwepo kwa kiambishi mwishoni mwa mzizi (a na wa). Kiambishi hicho hujitokeza mwishoni mwa kitenzi na kupelekea kupatikana kwa maana mbili kama sentesi zinavyojidhihirisha hapo chini.

(i) Alisema atakuchezea

Katika sentensi hii tunapata maana mbili ambazo ni: Maana ya kwanza mtu huyo atakuchezea wewe na maana ya pili mhusika huyo atamchezea.

(ii) Alisema atatembelewa

Katika sentesi hii zinajitokeza maana mbili ambazo ni (a) mtu huyo atatembelewa na sisi na (b) mtu huyo anaambiwa atatembelewa na watu wengine.

(iii) Kombo alisema hatoweza kukusaidia.

Katika sentensi hii zinapatikana maana mbili ambazo ni (a) Kombo ndie ambae hatoweza kukusaidia na (b) mtu mwengine (anayearifiwa na Kombo ) kuwa hatoweza kukusaidia.

(iv) Alisema amemsomea

Utata unaojitokeza katika sentensi hii ni pale maana mbili zinapojitokeza (a) habari ameisoma (b) habari hiyo hiyo amesomewa.

(v) Chungu kilichopikiwa

Sentesi hii ina kiambishi cha utendwa (wa) ambacho kinasababisha kupatikana maana mbili ambazo ni:  Maana ya kwanza inatuelekeza kwenye chungu kilichowahi kupikiwa na maana ya pili ni kuwa chungu sasa hivi kiko katika hali ya kupikiwa yaani kiko jikoni.

#### 4.2.2.6 Matumizi ya Viwakilishi –ake, oa

Data zinaonesha kuwa matumizi ya viwakilishi –ake- na-ao katika sentensi yanasababisha kujitokeza kwa utata katika sentensi za Kiswahili sanifu kama mifano inavyojidhihirisha hapo chini:

(i) Mama atashona nguo yake

Sentensi hii inadhihirisha maana mbili ambazo ni: (a) Nguo ni ya mama (b) mama ndiye atakayeishona nguo ya mtu mwengine.

(ii) Omar alimkamata paka wake.

Katika sentensi hii maana zinazopatikana ni paka aliyemkamata Omar ni wake mwenyewe na pili paka wa mtu mwingine amekamatwa na Omar.

(iii) Ali anachezea kichwa chake.

Sentensi hii ina maana mbili kwanza Ali anachezea kichwa chake mwenyewe na maana ya pili kichwa cha mtu mwingine kinachezewa na Ali.

(iv) Haroub alisema atafika kwao.

Sentesi hii inatupatia maana mbili, kwanza Haroub atafika anakokumiliki yeye na watu wengine na maana ya pili mtu mwingine atafika kwa Haroub.

(v) Ali atanunua mazao yao.

Sentensi hii inatupatia maana mbili zinapatikana ambazo ni Ali atanunua mazao ambayo ni ya kwao yanayomilikiwa na wao na ya pili Ali atanunua mazao yanayomilikiwa na wao na watu wengine.

**4.2.2.7 Utata Unaosababishwa na Mzizi – ingine-**

Data zinaendelea kuonyesha kuwa mzizi- ingine-unasababisha utata katika sentesi ambazo mzungumzaji anaweza kupata maana zaidi ya moja pale zinapotumika katika mawasiliano, kwa mfano:

(i) Kingine kimempotea. Maana ya kwanza inayopatikana ni -zaidi ya na maana ya pili ni badala ya.

(ii) Wengine hawatambuliki. Maana ya kwanza inayopatikana ni -zaidi ya na maana ya pili ni -baadhi ya naya tatu ni badala ya

(iii) Vingine havichukuliki. Maana ya kwanza ni -zaidi ya, ya pili ni-baadhi ya, ya tatu ni -badala ya.

(iv) Zingine zimeharibika. Maana ya kwanza ni -baadhi ya, ya pili -zaidi ya

(v) Nyingine zimepotea

Maana ya kwanza ni'baadhi ya' na ya pili ni 'zaidi ya' ata hizo hapo juu zinaendelea kuonyesha kuwa utata unapatikana tunapotumia mzizi –ingine- kwani katika sentesi (i) kingine kimepotea tunapata maana ya zaidi ya- au badala ya. Katika sentesi (ii)

wengine hawatabuliki inatupatia maana zaidi ya, baadhi ya, na badala ya. Vilevile sentensi (iii) vyengine havichukuliki inatupatia maana zaidi ya, baadhi ya, au badala ya na kupelekea kukwamisha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji.

#### 4.2.2.8 Matumizi ya Baadhi ya Viunganishi

Data zinaendelea kuonyesha kuwa matumizi ya baadhi ya viunganishi husababisha kujitokeza kwa utata katika sentensi pale vinapotumiwa vibaya. Kwa mfano:

(i) Nilikutana na kuku na vifaranga wake. Katika sentensi hii msomajianaweza kupata maana zaidi ya moja. Maana ya kwanza ni kuwa kuku aliandamana na vifaranga wake mwenyewe, ya pili ni kuwa nilikutana na kuku kisha nikakutana na vifaranga wa kuku mwingine.

(ii) Nilimsomesha Juma na ndugu zake, hapa maana ya kwanza ni nilimsomesha Juma na ndugu zake Juma, na yapili ni kuwa nilimsomesha Juma napia nimewasomesha ndugu wa mtu mwingine

(iii) Nilizungumza na mwalimu na wanafunzi, hapa tunapata maana ya kwanza kuwa nilizungumza na mwalimu na wanafunzi wake mwalimu na maana ya pili ni kuwa nilizungumza na mwalimu napia nilizungumza na wanafunzi wengine.

(iv) Nilitembea na bibi na jirani zake. Sentesi hii inatupatia maana ya kwanza tulitembea pamoja na mimi, bibi na jirani zake bibi. Na maana ya pili ni kuwa nilitembea na bibi kisha nikatembea na jirani wengine.

(v) Nilisoma na Asha na ndugu yake. Sentesi hii tunapata maana ya kwanza kuwa nilisoma na Asha na ndugu yake Asha kwa wakati mmoja. Na maana ya pili ni kuwa nilisoma na Asha napia nilisoma na ndugu yake mtu mwingine.

Mifano katika data i hadi v hapo juu inaonesha kuwa katika sentesi (i) Nilikutana na kuku na vifaranga vyake, tunapata maana ya kwanza kuku aliandamana na vifaranga wake mwenyewe. Vilevile maana nyingine nilikutana na kuku kisha nikakutana na vifaranga wa kuku mwingine. Katika sentesi (i) Nilimsomesha Juma na ndugu zake, tunapata maana ya kwanza nilisomesha Juma na ndugu zake Juma. Pia tunapata maana kuwa nilimsomesha Juma na nimewasomesha ndugu wa mtu mwengine.

#### 4.2.2.9 Matumizi ya Baadhi ya Vihusishi

Data zifuatazo zinaonyesha kuwa matumizi ya baadhi ya vihusishi husababishakujitokeza kwa utata katika sentensi za Kiswahili Sanifu. Kwa mfano:

(i) Baba anapenda kulima kuliko mama

(ii) Ali anacheza wakati wa mchana zaidi kuliko Said

(iii) Njiwa anapenda kuruka zaidi kuliko kuku

(iv) Baba anakula samaki kuliko nyama

(v) Mwalimu anamsifu Omar kuliko Salim.

Baba anapenda kulima kuliko mama, sentensi hii inapotumiwa na wazungumzaji inabainisha maana mbili ambazo ni baba anapenda kulima zaidi kuliko anavyompenda mama, baba anapenda kulima zaidi ya vile mama anavyopenda kulima.Ali anacheza wakati wa mchana zaidi kuliko Said, tunapata maana Ali anapenda kucheza wakati wa mchana zaidi kuliko Saidi na Saidi anacheza mchana lakini sio kama anavyocheza Ali. Njiwa anapenda kuruka zaidi kuliko kuku, sentesi hii inatupatia maana ya kwanza njiwa anapenda kuruka zaidi ya vile anavyopenda kuruka kuku na maana ya pili njiwa anapenda kuruka kuliko anavyompenda kuku. Sentensi baba anakula samaki kuliko nyama nayo inatupatia maana ya kwanza baba anapokula basi anakula samaki

na maana ya pili ni kwenye nyama na samaki, baba anakula samaki zaidi.Pia katika sentensi mwalimu anamsifu Omar kuliko Salim pia tunapata maana ya kwanza mwalimu anapenda kumsifu Omar zaidi ya vile anavyopenda kumsifu Salim na maana ya pili mwalimu anamsifu na anampenda Omar zaidi.

#### 4.2.2.10 Makosa ya Kisarufi na Kimantiki

Data zifuatazo hapo chini zinaendelea kuonyesha kuwa makosa ya kisarufi na kimantiki husababisha kujitokeza kwa utata katika sentesi za Kiswahili Sanifu. Kwa mfano:

(i) *Mwalimu ameondoka kazini*; katika sentesi hii inawezekana kuwa mwalimu ameondoka kwenda kazini au mwalimu meondoka hayupo tena kazinini

(ii) *Mwanafunzi wangu amerudi shuleni;* hapa tunapata maana mbili kwanza mwanafunzi amerudi kutoka shuleni, pili mwanafunzi amerudi tena kwa mara nyingine shuleni na tatu mwanafunzi haendi shuleni

(iii) *Saidi ameondoka chuoni*; katika sentesi hii zinapatikana maana mbili ambazo ni Saidi ameondoka hayupo tena chuoni na Saidi ameshahama chuo.

(iv) *Mwalimu anayesomesha ametokea nyumbani;* sentesi hii inatoa maana zifuatazo kwanza mwalimu anayesomesha ametokea nyumbani kwa mzungumzaji akaenda kusomesha; pili anamanisha kuwa huyo mwalimu na yeye wanatokea sehemu moja yaani kwao ni kumoja.

Sentensi (i) Mwalimu ameondoka kazini hii ina maana ameondoka kwenda kazini au hayupo tena kazini. Hali hii inasababishamawasiliano miongoni mwa wanajamii kushindwa kuwa ya ufanisi katika mazungumzo yao. Sentensi (ii) Mwanafunzi wangu

amerudi shule, hii inatupatia maana ya kuwa mwanafunzi amerudi kutoka shuleni au amerudi tena kwa mara nyingine.

Baada ya kupata tungo tata mtafiti alitumia mbinu ya dodoso na hojaji ili kupata data za tafsiri ya tungo hizo kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Katika kufanya hivyo, mtafiti aliwapa wahojiwa dodoso lenye lengo la kuwataka watafsiri sentensi hizo kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.Mtafiti aliwauliza watafitiwa tajwa katika utafiti huu kama wanaelewa aina za tungo zenye utata katika lugha ya Kiswahili sanifu zenye changamoto ya kutafsiri kwenda lugha ya Kiingereza.Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, Asilimia 93ya watafitiwa walikubali kuwa wanaelewa ainaza tungo zenye utata katika lugha ya Kiswahili sanifu zenye changamoto ya kutafsiri kwenda lugha ya Kiingereza.

Aidha katika hojaji watafitiwa waliulizwa swali lenye lengo la kubainisha uelewa wao juu ya tungo tata na aina zake. Swali hilo lilisema Kama unazielewa, je unakubali kuwa aina hizo za tungo ni tungo neno, tungo kirai, tungo kishazi na tungo sentensi. Kwa kutumia swali hilo, mtafiti alilenga kupata uelewa wa watafitiwa kuhusu tungo tata na pia wazibainishe kulingana na makundi yake. Matokeo yalionesha kuwa baadhi ya tungo hizo ziko katika ngazi ya neno na baadhi ya tungo hizo ziko katika ngazi ya sentensi.Kwa mfano,katika ngazi ya neno,kuna tungo kama vile, “paa” yenye maana zifuatazo; sehemu ya juu ya nyumba,mnyama, anaefanana na mbuzi,tendo la kwenda juu, chukua baadhi ya makaa ya moto kutoka mekoni, na ondoa magamba ya samaki kwa kuparuza kwa kitu (tazama pia katika TUKI: 2012:445).

Katika dodoso watafitiwa walitoa mifano ya sentensi kama vile, “mtoto anaendesha”, yenye maana zifuatazo; anaendesha chombo cha usafiri kama vile meli barabarani,

tenda tendo la kumdhalilisha mtu mwingine, anaharisha, na anampeleka mtu mahali kwa chombo cha usafiri (TUKI; 2012:98). Sentensi zingine zenye utata walizozitaja ni; ananichezea mwanangu, amelalia uji, na niletee mbuzi; chimbuko la utata wa tungo hizi ni tungo katika ngazi ya neno kama vile, ananichezea, amelalia, na mbuzi, tungo hizi zina maana zaidi ya moja kama ifuatavyo:

Tungo sentensi "Ananichezea mwanangu"linaweza kuwa na maana kama vile, anamloga mtoto wangu,anamfunda mtoto wa kike kwa niaba ya mzazi kwa mujibu wa mila za watu husika kama sehemu ya mafunzo ya kujiandaa kuolewa, yupo mtu anayecheza kwa niaba ya mtoto wake, na yupo mtu anayecheza kumfurahisha mtoto wake (TUKI; 2012:65).

Tungo sentensi "Amelalia uji" linaweza kuwa na maana kama vile, kulala juu ya uji, kutwa nzima kashinda kanywa uji tu mpaka amelala. Tungo sentensi "Niletee mbuzi" linaweza kuwa na maana kama vile, chombo cha kukunia nazi, mnyama afugwae.Tungo sentensi "Niletee nyanya" linaweza kuwa na maana kama vile, niletee nyanya (tunda/kiungo), niletee bibi wa baba au mama, niletee mti wa mnyanya.

Kwa mujibu TUKI (1990:4), utata ina maanisha hali ya kipashio fulani kuweza kueleweka kwa maana zaidi ya moja. Aidha TUKI (2012:614) wanaeleza kuwa utata una maanisha ugumuwa kueleweka kitu.Kwa mitarafu ya utafiti huu, utata ni hali ya kipashio fulani kuweza kueleweka kwa maana zaidi ya moja. Aidha kwa mujibu wa TUKI 1990:16) tungo (construction) inamaanisha matokeo ya kupanga pamoja vipashio sahili ili ili kujenga vipashio vikubwa zaidi. Hivyo, kwa mkabala wa sarufi miundo, tungo tata zinaweza kuwa katika ngazi ya neno na ngazi ya sentensi.

Tungo huanzia katika ngazi ya neno na kufuata kipashio kikubwa zaidi ya neno ambacho ni kirai, kisha kishazi na kuishia sentensi. Hivyo aina kuu za tungo tata pia hupatikana katika ngazi hizi za neno, kirai, kishazi, na sentensi. Matokeo ya utafiti hapo juu yamedhihirisha kuwa aina za tungo zipo katika ngazi hizo. Baadhi ya utata tumeona kuwa unapatikana kutokana na neno,mwingine unatokana na kishazi kama vile "***Ali ametumwa na Kombo"***na mwingine katika ngazi ya sentensi kama vile "***.Kaka yako amerudi kazini".***Kwa mujibu wa Mwansoko(1996:2) moja ya aina za tungo zenye utata ni zile tungo katika ngazi ya neno.Tungo hizi zinaweza kuleta utenge katika tafsiri nakusababisha **hasara** kubwa.

Kwa mfano, inasemekana mlipuko wa mabomu ya atomiki ya huko Japani ulisababishwa na tafsiri tenge ya neno la Kijapan 'MOKASUTU**"** katika simu ya maandishi (telegramu) iliyopelekwa Washington D.C. kutoka Japani ((Mwansoko, keshatajwa). Neno hilo lilitafsiriwa kwa makosa kuwa **"*Ignored*"** badala ya "***Considered"*** (Mwansoko, keshatajwa). Hali hii inaweza kutokea pia katika lugha ya Kiswahili ambayo imetudhihirishia kuwa na maneno ambayo yanaweza kuwa na fahiwa zaidi ya moja kutegemeana na muktadha wa matini husika. Kutokana na hali hiyo, endapo mfasiri hana uelewa mpana katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza, huweza kutafsiri neno la Kiswahili visivyo katika lugha ya Kiingereza.

Kwa hiyo, aina ya tungo neno na tungo sentensi za lugha ya Kiswahili zinaweza kuleta changamoto sana katika tafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.Hii inatokananatafsiri tenge ya mawazo kutoka lugha chanzo ya Kiswahili kwenda lugha lengwa ya Kiingereza.Kwa hiyo, data za utafiti huu zilidhihirisha kuwa sentensi/ tungo za Kiswahili zina utata na utata huo unaweza kuathiri

mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kiswahili. Athari hiyo huwa ni katika uibuaji wa maana kwa msikilizaji ama msomaji ambaye anaweza asipate maana halisi iliyokusudiwa na msemaji ama mwandishi wa sentensi hiyo.

Aidha, utafiti huu uliona kuwa muktadha wa matumizi ya sentensi ni wa muhimu sana katika kupata maana iliyokusidiwa na msemaji ama mwandishi wa sentensi yenye utata. Hata hivyo, swali likabaki ni kwa namna gani sentensi/tungo zenye utata zinaweza kutafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na changamoto zake ni zipi katika mawasiliano. Swali hili lilitupeleka katika lengo la pili la utafiti huu ambalo lililenga kubainisha changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata na atahri zake katika mawasiliano. Sehemu ifuatayo ianwasilisha, kuchambua na kujadili data zilizopatikana katika kufikia lengo hilo.

## 4.3 Changamoto za Kutafsiri Tungo na AthariZake katika Mawasiliano

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha changamoto za kutafsiri tungo tata na athari zake katika mawasiliano. Kwa kutumia mbinu ya dodoso na hojaji mtafiti alikusanya data zinazoonesha changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata. Katika dodoso wahojiwa waliulizwa maswali matatu yenye lengo la kubaini changamoto za kutafsiri sentensi/tungo zenye utata kama ifuatavyo.

Kwanza walitakiwa kubainisha endapo kuna changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata, pili wahojiwa walitakiwa kutajachangamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na nne waeleze athari za changamoto hizo katika mawasiliano. Matokeo yalikuwa kamayanavyojidhihirisha katika sehemu zifuatazo:

### 4.3.1 Uwepo wa Changamoto za Kutafsiri Sentensi Zenye Utata

Katika utafiti huu wahojiwa waliulizwa endapo kuna changamoto za kutafsiri tungo zenye utata kutoka lugha ya Kiswahili kwenda katia lugha ya Kiingereza na athari zake katika mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha hizo mbili. Katika kujibu swali hilo wahojiwa walitakiwa kujibu ndiyo au hapana. Matokeo yalikuwa kama yanavyojidhihirisha katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 4.1: Kuwepo kwa Changamoto za Kutafsiri Tungo Tata**

| Na. | Ndiyo | Hapana |
|---|---|---|
| Wanafunzi chuo kikuu | 50 | 10 |
| Wanafunzi sekondari | 10 | 10 |
| Wahadhiri | 5 | 0 |
| Walimu sekondari | 10 | 0 |
| Wafasiri | 5 | 0 |
| **Jumla** | **80** | **20** |

Chanzo: Data za utafiti (June, 2016)

Data katika jedwali hapo juu zinaonesha kuwa, watafitiwa 80walisema ndiyo kuna changamoto katika kutafsiri tungo tata za lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza wakati watafitiwa 20 walisema 'hapana' na hakuna mtafitiwa aliyesema hajui. Matokeo haya yanaonesha kuwa tafsiri ya sentensi/tungo zenye utata kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kiingereza kuna changamoto ambazo mfasiri anaweza kukumbana nazo na pia msomaji wa matini lengwa. Hii inaonesha kuwa kila lugha ina kanuni zake na taratibu zake katika kuibua maana za maneno ya lugha hiyo. Kwa hiyo, Kiswahili naKiingereza ni lugha mbili zinazotofautiana na toafuti hizi huweza kujidhihirisha katika semantiki ya lugha hizo. Uibuaji wa maana hutokana na maneno na muktadha wa matumizi ya maneno hayo

katika lugha. Kwa misingi hiyo, sentensi ama tungo inapokuwa na utata katika lugha chanzi inaleta ugumu kuhamisha maana lengwa katika lugha lengwa.

### 4.3.2 Changamoto za Kutafsiri Sentensi Zenye Utata

Kama ilivyoelezwa watafitiwa walitakiwa kutaja changamoto za kutafsiri tungo tata hizo. Majibu ya watafitiwa yalionesha kuwa changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata ni kama ifuatavyo:

(i) Changamoto za kiutamaduni

(ii) Ukosefu wa visawe

(iii) Changamoto za muktadha na mazingira

(iv) Changamoto za wakati

(v) Changamoto za kiisimu

(vi) Changamoto za kimaana na kimuundo

Kutokana na majibu ya wahojiwa utafiti huu ulibaini kuwa changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata kutoka katika Kiswahili kwenda katika Kiingereza ni pamoja na changamoto za kiutamaduni, ukosefu wa visawe, muktadha na mazingira, kiisimu, kiwakati na kimaana na muundo. Sehemu ifuatayo inajadili changamoto hizo kwa kutumia mifano

#### 4.3.2.1 Changamoto za Tofauti za Kiutamaduni

Tafiti mbalimbali zikiwemo za Mwangi (2016)na Petre (2012), zinadhihirisha kuwa changamoto katika kutafsiri matini zenye tungo tata kutoka lugha mbalimbali kwenda lugha nyingine ni paomoja na zile zilizotajwa hapo juu. Matokeo ya utafiti wetu huu yanashabihiana na matokeo ya tafiti hizo pamoja na kauli za kinadharia kuhusu

changamoto hizo zinozodai kuwa changamoto nyingi zinatokana na tofauti za kiutamaduni kati yajamii moja na nyingine zenye kuongea Kiswahili na zile zenye kuongea Kiingereza. Kwa mfano, dhana ya joto na baridi katika tafsiri ya tungo kama vile, "ubaridi na ujoto, unene na wembamba, utata kuhusu uzuri wa sura katika jamii hizi mbili tofauti, na mengine mengi. Kwa mfano watafitiwa walibainisha sentensi zifuatazo;

(i) Kata mbili 'Cut two'

(ii) Juma ana paa 'Juma has a roof'

(iii) Musa ana paka 'Musa has a cat'

Ukichunguza sentensi katika mfano namba i hadi iii utaona kuwa ni tungo tata zenye maana zaidi ya moja. Maana ya sentensi hizo inategemea mkutadha wa utumizi. Kwa hiyo, endapo mfasiri atashindwa kubainisha tofafuti za kiutamduni za lugha hizi mbili anaweza kushindwa kufikisha ujumbe sahihi na hivyo kupoteza maana ya lugha chanzi. Kwa mfano, neno 'kata' katika jamii ya Kiswahili ni neno linalorejelea dhana tatu kwanza kama dhana ya kiutamaduni ni kifaa cha kutekea ama kunywea maji na pia katika muktahda mwingine ni kitendo cha kukata kitu na vilevile ni eneo la kiutawala. Kwa hiyo, mfasiri asiyejua utamaduni wamswahili anaweza kutafsiri kama kitendo badala ya kifaa au eneo la kiutawala.

Mfano mwingine ni Juma ana paa mfasiri anaweza kupotosha maana ama ujumbe wa matini chanzi pale anapoweza kutafsiri paa kama paa la nyumba ama mnyama. Katika utamaduni wa mswahili muktadha humruhusu msemaji kutumia neno paa kama sitiari ya ushindi ama uwezo wa kufanya jambo hapo anaweza kusema juma ana paa akiwa na maana juma anakwenda vizuri katika maendeleo ya jambo fulani. Kwa hiyo, kwa

mafsiri asiye na uelewa wa utamaduni huu anaweza kushindwa kubaini maana na ujumbe lengwa badala ya kusema *Juma is fliying* akasemaJuma has a roof.

**4.3.2.2 Changamoto za Ukosefu waVisawe**

Kwanza ni kukosekana kwa vibadala katika lugha ya Kiingereza vinavyolingana na vile vinavyopatikana katika Kiswahili sanifu. Hali hii husababisha ugumu wa kutafsi sentensizenye utata kutoka lugha hizo. Kwa mfano:

(i) Said amenunua mbuzi,

Neno mbuzi katika Kiswahili sanifu linamaanisha kuwa ni mnyama au kifaa cha kukunia nazi nyumbani, katika lugha ya Kiingereza hakuna kibadala cha neno mbuzi tunapata mbuzi mnyama tu (goat). Kwa mfano, sentesi ya Kiingereza *Said bought a goat*. Sentesi hii inatoa maana ya mbuzi mnyama kinyume na ile ya Kiswahili ambayo hutupatia maana mbili tofauti.

(i) *Kata* ambalo linapotumiwa katika Kiswahili hutoa maana nyingi. Katika sentesi 'Niletee kata' tunapata tafsiri nyingi kwa mfano kata ya kuchota maji, kata ya kukata kitu, kata ya kujitwishia kichwani. Kwenye Kiingereza hutumika neno 'cut' lenye maana moja ya kitendo cha kukata kitu nakusababishaugumu wa kutafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza au kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

(ii) Amepata jiko.

Katika sentensi hiyo tunapata tafsiri ya jiko la kupikia, sehemu ya kupikia ama kuoa mke. Changamoto inayopatikana ni kuwa unapoitafsiri sentensi hii kwa Kiingereza neno jiko linatoa tafsiri moja tu ambapo sentensi inakuwa *she has got a cooker*. Hapa

haina utata kwani cooker ya Kiingereza haiwezi kutumika kama ilivyotumika katika Kiswahili.

(iii) Juma amelalia mkaa

Katika sentensi namba (iii) hapo juu, tunapata maana ya kwanza Juma amelala juu ya mkaa au Juma amekula mkaa kama chakula cha usiku. Kwenye Kiingereza mkaa ni charcoal ina maana moja tu ambapo tunapata sentensi *Juma sleeps on charcoal*.

(i) Neno “choma” lina maana ya kuteketeza, kudunga, kitendo cha kuivisha chakulakwenye moto lakini neno choma kwa Kiingereza ni *burn* ambalo hutoa maana moja tu.

(ii) Neno “kichwa”kwenye Kiswahili lina maana ya kiongozi, sehemu ya mwili ya mtu au mnyama ambapo kwenye Kiingereza kichwa ni *head* na hutoa maana moja tu.

(iii) Neno “Zima” maana zake ni sehemu kamili ya kitu, kufanya moto usiendelee kuwaka na kua kwa maana ya kuondoa uhai wa kiumbe.Neno hil hili kwa Kiingereza ni switch off kwa maana ya kuzima taa, redio au kitu kingine.

#### 4.3.2.3Changamoto za Muktadha na Mazingira

Changamoto ya mazingira ni moja ya changamoto iliyojidhihirisha katika utafiti huu. Data zilionesha kuwa kuna changamoto ambazo zinatokana na mazingira wakati wa kutafsiri. Kwa mfano ukisema Juma ana paka. Katika sentensi hii tunaona kuwa katika lugha ya Kiswahili mwandishi anaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Paka katika Kiswahili inaweza kurejelea paka mnyama na paka kitendo. Mfasiri anaweza kushindwa kutafsiri sentensi hiyo kulingana na ujumbe uliokusudiwa na hivyo kuitafsiri kama paka juma has a cat. Badala ya juma is painting. Asilimia 90 ya

wahojiwa walitafsiri kamajuma has a cat. Hii inadhihirisha kwamba muktadha katika tafsiri ya matini za sentensi tata unahitajika sana ili kufanikisha mawasiliano.

#### 4.3.2.3 Changamoto ya Kimuktadha na Matumizi

Muktadha na matumizi ni changamoto ambayo ilionekana kuathiri tafsiri ya sentensi zenye utata na mawasiliano kwa ujumla. Utafiti huu ulibaini kuwa, muktadha unaweza kuwa wakawaida au wa kifasihi. Kwa mfano:

(i) Amelalia uji

Katika sentensi hiyo tunaona kuwa ina maana zaidi ya moja ambapo ina maana amelala akiwa amekunywa uji tu bila kula chakula chochote ama amelala juu ya uji.Changamoto kubwa inapatikana kwa kutafsiri kwa Kiingereza.

Kwa kuangalia maneno kama anaendesha katika hali ya kawaida anaendesha kipando kama gari, baiskeli, honda nakadhalika, kwa muktadha wa tafsida neno anaendesha nikuwa ana harisha. Kwa maana hiyo neno anaendesha ni changamoto kulitafsiri kwa Kiingereza kwani halina utata linakuwa ni driving na kuharisha neno lingine kabisa. Neno anapanda lenye maana ya kuotesha mazao, kupanda miti au mimea, kupanda juu lina changamoto kulitafsiri ambapo kwenye Kiingereza lina maana moja tu.

(i) Neno anapaa

Tunapata maana ya neno anapaa kwakuangalia muktadha wa kawaida na wa kifasihi. Maana tunazozipata ni anapaa angani na pia anapaa moto kwa hali hiyo huwezi kupata neno la Kiingereza linaloweza kutumika kama linavyotumika neno la Kiswahili kwa hiyo nayo ni changamoto.Said amevaa miwani.Katika hali ya kawaida Saidi amevaa miwani ya kuonea. Pia katika mazingira ya kifasihi Saidi amevaa

miwani nikuwa yuko mazingira ya baa ambapo unasema saidi amelewa pombe.Tukiifasiri kwa Kiingereza tunasema Saidi wears glasses.Kwa maana ya kuvaa miwani nasio kulewa kama inavyoonekana kwenye Kiswahili.

#### 4.3.2.4 Tofauti za Kimaeneo

Changamoto ya kutafsiri tungo za Kiswahili zenye utata kwenda Kiingereza pia zinapatikana kwenye tofauti ya kimaeneo au za kilahaja.Kwa mfano:

(i) Ali amesimama karibu na mfereji.

Sentensi hii ukiwapa watu wa Zanzibar na Tanzania bara watakupa maana tofauti. Mfereji inatumika Zanzibar na Tanzania bara wanatumia neno bomba. Kutafsiri kwa Kiingereza bomba na mfereji zote ni tap, hakuna neno jingine ambalo mfasiri unatakiwa pia ujue asili ya mwandishi.

(i) Amevaa kozi na gubi

Neno kozi na gubi yana maana sawa ambapo maana ya kuti kavu la mnazi linalokwanyuka kutoka juu.Kutokana na tofauti za kieneo Zanzibar linaitwa kozi na Pemba linaitwaa gubi, changamoto inakuwepo unapotafsiri maneno kama haya yenye tofauti za kimaeneo.

(i) Tukiangalia tena neno bibi na nyanya zenye maana sawa lakini zinatamkwa tofauti kutokana na tofauti za kimaeneo ambazo nazo zinaleta changamoto kubwa kutafsiri kwenye lugha ya Kiingereza.

#### 4.3.2.5 Changamoto ya Miundo ya Kisarufi

Miundo ya kisarufihutoa changamoto katika kutafsiri tungo yenye utata kwenda Kiingereza. Kwa mfano:

(i) Asha alitumwa na Juma.

Sentensi namba i. hapo juu ni sentensi tata yenye maana zaidi ya moja kutokana na muundo wake wa kisarufi. Maana tunazozipata hapa ni kwamba; Juma amemtuma Asha yaani Asha anamtumikia Juma. Maana ya pili nikuwa Asha na Juma wametumwa pamoja. Maana hizi mbili zinaleta changamoto kuweza kuitafsiri kwa lugha ya Kiingereza. Tafsiri inaweza kufanyika kwa kutumia maana moja na hivyo kupoteza maana na ujumbe uliokusudiwa katika matini chanzi na hivyo kuharibu mawasiliano.

(i) Amepigwa na bibi.

Katika sentensi namba 11 hapo juu inatupa maana zaidi ya moja yaani; bibi ndiye aliyempiga, au yeye na bibi wamepigwa. Sentensi hii ina muundo tata ambao katika tafsiri mfasiri anaweza kushindwa kuitafsiri kwa ukamilifu wake kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na hivyo kuharibu ufanisi wa mawasiliano.

(i) Asha amemuandikia Omar barua,

Sentensi namba iii kwa Kiingereza she writes a letter for Omar. Sentensi ya Kiswahili ina maana zaidi ya moja na tunapata maana kuwa Asha ameandika barua kwenda kwa Omar. Pia maana nyengine nikuwa Asha ameandika barua kwa niaba ya Omar.Sentensi hiyo ya Kiingereza inaeleweka haina utata neno writes ni kuandika haina maana nyengine kama ilivyo kwenye Kiswahili. Sentensi nyingine amelala kwenye nyumba ya wageni, Sentensi hii ya Kiswahili huweza kumaanisha nyumba ya mtu, lakini inatumika kwa ajili ya wageni kwa malipo au ni nyumba inayo milikiwa na watu ambao ni wageni katika eneo lile. Sentensi ya Kiingereza haina utata gest house ndilo neno linalotumika kuwa ni nyumba ya wageni hakuna utata.

### 4.3.3 Athari za Changamoto za Tafsiri ya Sentensi Tata katika Mawasiliano

Utafiti huu ulibaini kuwa tafsiri ya sentensi tata ina athari katika mawasiliano. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba asilimia (85%) ya watafitiwa walitaja athari hizo kuwa ni pamoja na;

(i) Upotofu wa maana na ujumbe wa awali. Wahojiwa walibainisha kuwa matatizo ya kutafsiri sentensi tata huweza kumfanya mfasiri akapotosha maana ama ujumbe wa matini chanzi katika matini lengwa na hivyo kuharibu mawasiliano.

(ii) Kupotosha muundo wa sentensi ya matini chanzi. Wahojiwa walibainsiha kuwa muundo wa sentensi ya matini chanzi unapoharibiwa katika tafsiri tenge huweza kuharibu maana na ujumbe wa matini chanzi katika matinini lengwa.

(iii) Kukosekana kwa ushikamani wa ujumbe. Wahojiwa walibainisha kuwa mfasiri anaposhindwa kutafsiri sentensi zenye utata huweza kuharibu ushikamani wa ujumbe wa matini chanzi katika matini lengwa.

(iv) Kukosekana kwa ushikamani wa maana baina ya matini chanzi na matini lengwa. Mawasiliano fanisi hukosekana baina ya hizi jamii mbili kutokana na kuhawilisha maana potofu katika lugha ya Kiswahili kwenda katika Lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa wana nadharia za tafsiri na ufasiri (Mshindo, 2010, Mwansoko, 1996, Newman, 1969), madhara yanayoweza kutokea kutokana na utata huu ni ya kufanya tafsiri tenge. Tafsiri tenge, huweza kusababisha hasara kubwa katika jamii kwa kupotosha maana iliyokusudiwa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Athari nyingine inayoweza kusababishwa na utata ni pamoja na ugumu wa kujifunza lugha hasa kwa wageni.

Kwahiyo athari ya tungo zenye utata za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda lugha ya Kiingereza katika mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji walugha hizo imeonekana kuwa kimsingi husababishwa na tafsiri tenge.

## 4.4 Muhtasari

Sura hii ilihusu uwasilishaji wadata na mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura hii imewasilisha na kujadili data kuhusu aina ya tungo tata katika Kiswahili. Aidha,ni katika sura hii ambapo data utafiti zimewasilishwa katika mtindo wa kitakwimu ambapo majedwali yametumika katika uwasilishaji huo. Vilevile, data hizo zimeweza kuchambuliwa kwa kutolewa maelezo ya kina kulingana na maswali ya utafiti yalivyouliza. Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba asilimia 93 ya watafitiwa wanaelewa kuwepo kwa tungo zenye utata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

Asilimia 92 walijibu swali la pili na kueleza kwamba wanaelewa utata unaweza kujitokeza katika neno, kirai, kishazi na katika sentesi. Aidha, asilimia 80 walieleza kuwepo kwa changamoto za kutafsiri sentensi hizo kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ilihali asilimia 85 walionesha kuwepo kwa athari mbali mbali za tungo zenye utata za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda Kiingereza.

Aidha sura hii imebainisha kuwa kuna changamoto katika kuatafsiri sentensi zenye utata ambapo imeelezwa kuwa changamoto hizo ni za kiutamaduni, ukosefu wa visawe, kimuktadha na mazingira, kimuundo na kimaana pamoja na tofauti za kimaeneo. Utafiti huu umebaini kuwa tafsiri ya sentensi zenye utata husababisha matatizo na kuathiri mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji na wasomaji wa

lugha zote mbili. Athari za changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata hujidhihirisha katika upotofu wa maana na ujumbe, upotoshaji wa muundo wa sentensi ya matini chanzi, kukosekana kwa ushikamani wa ujumbe na kukosekana kwa ushikamani wa maana na ujumbe.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Baada ya mchakato mzima wa kukamilisha utafiti huu, sura hii imetoa majumuisho ya hatua zote za utafiti juu ya mambo ambayo yamebainika. Aidha, imetoa mapendekezo muhimu ambayo yanatarajiwa kuwa muongozo kwa watafiti wengine, watakaopenda kufanya utafiti juu uchambuzi wa changamoto za kutafsiri sentensi tata za Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza.

## 5.2 Muhtasari

Katika uwasilishaji na uchambuzi wa data, data zinaonesha kuwa lengo kuu la utafiti ni kubainisha changamoto za kutafsiri sentensi tata kutoka Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza. Utafiti una malengo mahususi matatu, lengo la kwanza ni kubainisha aina za utata katika sentensi za Kiswahili sanifu, la pili ni kubainisha utata katika Kiswahili Sanifu na la tatu ni kubainisha sentensi zenye utata katika Kiswahili Sanifu zenye changamoto ya kutafsiri kwenda Kiingereza.

Data zimechanganuliwa kwa kutumia Nadahria ya Ulinganifu wa Kimuundo ya Cartford (1965). Uchambuzi wa data unaendelea kuonyesha kuwa utata unaweza kusababishwa na neno kuwa na maana zaidi ya moja, kutozingatia taratibu za uandishi, utumiaji wa maneno bila kuzingatia muktadha, utumiaji wa maneno yenye maana ya picha, kujitokeza kwa kauli ya kutendea, kujitokeza kwa matumizi ya vimilikishi –ake- na –ao-, matumizi ya mzizi -ingine-, matumizi ya baadhi ya viunganishi na baadhi ya vihusishi na makosa ya kimantiki na kisarufi.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba asilimia 93 ya watafitiwa wanaelewa kuwepo kwa tungo zenye utata kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Asilimia 92 walijibu swali la pili na kueleza kwamba wanaelewa utata unaweza kujitokeza katika neno, kirai, kishazi na katika sentesi. Aidha asilimia 80 walieleza kuwepo kwa changamoto za kutafsiri sentensi hizo kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ilihali asilimia 85 walionesha kuwepo kwa athari mbalimbali za tungo zenye utata za Kiswahili zilizotafsiriwa kwenda Kiingereza. Aidha sura hii imebainisha kuwa kuna changamoto katika kutafsiri sentensi zenye utata ambapo imeelezwa kuwa changamoto hizo ni za kiutamaduni, ukosefu wa visawe, kimuktadha na mazingira, kimuundo na kimaana pamoja na tofauti za kimaeneo. Utafiti huu umebaini kuwa tafsiri ya sentensi zenye utata husababisha matatizo na kuathiri mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji na wasomaji wa lugha zote mbili.

Athari za changamoto za kutafsiri sentensi zenye utata hujidhihirisha katika upotofu wa maana na ujumbe, upotoshaji wa muundo wa sentensi ya matini chanzi, kukosekana kwa ushikamani wa ujumbe na kukosekana kwa ushikamani wa maana na ujumbe.Vilevile tofauti za kimaeneo au za kilahaja kwa mfano neno hutumika sehemu fulani tu na kutoa maana nyingi na mwisho changamoto inayosababishwa na miundo ya tungo za Kiswahili sanifu. Changamoto hizi husababisha ugumu wa kutafsiri sentensi tata za Kiswahili kwanda Kiingereza.

## 5.3 Hitimisho

Data zimechanganuliwa na kuonesha kuwa kuna changamoto za kutafsiri sentensi tata za Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza. Data zimebainisha changamoto mbalimbali ambazo ni kukosekana kwa vibadala katika Kiingereza ambavyo hupatikana katika

Kiswahili sanifu. Data zimeonyesha kuwa katika Kiswahili sanifu hupatikana vibadala vinavyotoa tafsiri nyingi za maneno, kwa mfano neno mbuzi hutoa maana ya mbuzi mnyama na mbuzi kifaa cha kukunia nazi, ambapo katika Kiingereza huwa na maana ya mnyama tu.

Data zimeendelea kuonesha changamoto nyingine ambayo inatokana na utamaduni, hujitokeza pale baadhi ya maneno hutumika zaidi kiutamaduni na kusababisha kupatikana kwa maana nyingi katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano Kiswahili sanifu hutumia mama mdogo na mama mkubwa wakati Kiingereza hutumia aunt kwa wote wawili.

Changamoto nyingine ni tofauti za kimaeneo na kusababisha tafsiri kuwa ngumu katika Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza. Changamoto nyingine miundo ya kisarufi ya Kiswahili sanifu inatofautiana na Kiingereza na kusababisha maana zaidi ya moja wakati wa kutafsiri.

## 5.4 Mapendekezo

Baada ya uchambuzi wa kina kazi hii ya utafiti imempa mtafiti mwanga wa kuweza kupata mawazo yaliyomfanya aibuke na mapendekezo ambayo yataamsha ari na hamasa kwa watafiti wengine wenye lengo la kufanya utafiti kuhusu tafsiri. Mtafiti amechambua changamoto za kutafusiri sentensi zenye utata za Kiswahili sanifu kwenda Kiingereza, mtafiti amependekeza kuwa watafiti wa Isimu wafanye tafiti nyingi zinazohusu changamoto za kutafsiri sentensi tata kutoka Kiswahili sanifu kwenda lahaja za Kiswahili. Pia amependekeza kuwa watafiti wengine wachambue

changamoto za kutafsiri sentensi tata za Kiswahili sanifu kwenda lugha za Kibantu, mwisho amependekeza kufanywe tafiti nyingi za Isimu kuhusu tafsiri kwa lengo la kupata marejeo zaidi.

## MAREJELEO

Atlas, J. D. (1989). *Philosophy without Ambiguity: A Logical Linguistic Essay.* Oxford: Oxford University Press

BAKITA, (2004). *Tafsiri Sanifu ,(Toleo na 6).* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Batibo, H. M. (1984). *"Tafsiri katika Vyumbo vya Habari".Makala katika Kiswahili na Vyombo vya habari,* S.A.K Mlacha (Mh,) Dar es Salaam:Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Chakata, (2013). Kongamano la Kimataifa la Kiswahili: Chuo Kikuu Cha Kikatoliki Cha Afrika Mashariki. Nairobi Kenya.

Cruse, A. (2011). *Meaning in Language. An introduction to semantics Pragmatics. 3rdEd.* Oxford University Press: New York.

East African Education Publishers, (2008). *Mtawa Mweusi:*Nairobi: Sitima Prin Stationers Ltd

Jilala, H. (2017). Changamoto za Kutafsiri Matini za Kiutamaduni katika Jamii Ulumbi: Mifano kutoka Tafsiri ya Majina katika Matini za Kitalii. Eldoret. *Mwanga wa Lugha. Juzuu 1(1),* 77 – 98.

Jilala, H. (2016). Tathmini ya Hatua za Tafsiri kama Nyenzo ya Ufanisi wa Mawasiliano. Dar es Salaam. *Kiswahili Journal. Juzuu 79(2*), 115-136.

Jilala, H. (mh.) (2016). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi.* Dar es Salaam. Daud Publishing Company Limited.

Jilala, H. (2016). *Uhakiki wa Nadharia ya Skopos katika Tafsiri:* Mifano yaTafsiri ya Matini za Kiutamaduni.katika Jilala, H. (Mh.). Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited.

Jilala, H. (2016). *Tathmini ya Utumizi wa Mbinu za Newmark (1988) katika Kutafsiri Matini za Kiutamaduni.* Katika Jilala, H. (Mh.) Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi. Dar es Salaam. Daud Publishing Company Limited.

Jilala, H. (2016). *Uchambuzi wa Nadharia ya Ulinganifu katika Fasihi.* Katika Jilala, H. (Mh.) Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi. Dar es Salaam: DaudPublishing Company Limited.

Khalfan, S. S. (2015). Tafauti za Sentensi za Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Dar es University Press.

Kihore, Y. M. (1991). "Miundo ya Kisarufi Taasisi Matatizo ya utatuzi".Makala ya Semina ya wasafiri wa Kiswahili.Desemba 16-21, 1991.

Malangwa, S. P. (2005). Problems of Translating Literary Works: The Case of JuliusKambarage Nyerere's Translation of The Play Mabepari wa Venisi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Malangwa, S. P. (2010). "Handling Technical Translations: The Case of Translation of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies.Theories and Application*. London: Routledge

Mutasa, V. E. (1999). Problems of Translation of Newspaper Articles.Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Mwansoko, H. J. M. (2006).*Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Dar es Salaam: TUKI.

Mtui, J. A. (2009). The Adequacy of Translation Theory with Respect to Drama: The Case of Samwel Mushi's Mfalme Edipode. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translaton.* London: Prentice Hall.

Nida, A. E., na Taber, C. R. (1969). *The Theory and Practice of Translation.* London: Prentice Hall.

Njenga, G. W. (2014). *Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria: Tathmini ya Katiba ya Kenya (2010).*Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oxford Dictionary, (2010). *Oxford Advanced Learner's Dictionary of Current English.* New York: Oxford University Press**.**

Ruhumbika, G. (1978). *"Tafsiri za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili" Makala kwenye Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili Dar es Salaam*. Dar es Salaam: TUKI.

Solomon, B. (2014). Utata wa Tungo na Namna ya Kuuepuka. Makala: Imepakuliwa tarehe 12/7/2016 kutoka: Mwannchi.co.tz.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi-Kenya: Focus: Publication Ltd.

Wathion'g N. (1968). *Black Hermit.* Kampala: East African EducationalPublishers Stationers Ltd.

Williamson, T. (1994). *Vagueness.* London: Routledge.

# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho Na. I: Orodha ya Sentensi Tata Katika Kiswahili Sanifu

| Na. | Sentensi (LC) | Sentensi (LL) |
|---|---|---|
| 1. | Amevunja ungo. | He broke ungo. |
| 2. | Asha amekula dawa chungu. | Asha has eaten a painful drug. |
| 3. | Mtoto mdogo amepanda juu ya mti | A little baby has climbed on a tree. |
| 4. | Juma ametengeneza panda. | Juma has made a panda. |
| 5. | Ametuletea kata mpya. | He has brought us a new ward. |
| 6. | Ameleta kanga. | He brought a Kanga. |
| 7. | Amefungia mpira. | He has closed the ball. |
| 8. | Juma amekanyaga waya. | Juma has wrapped the wire. |
| 9. | Mwalimu kakaa na ua zuri. | The teacher sat with beautiful flower. |
| 10. | Ali kaonekana mbuzi. | Ali has been seen goat. |
| 11. | Amenipigia ngoma. | Has played the drum/dance |
| 12. | Amempiga paa. | He/she hit a roof |
| 13. | Amelalia uji. | He sleept on the porridge. |
| 14. | Ananichezea mwanangu. | He/she  is playing my child. |
| 15. | Amechimba barabara | He/she has digthe road. |
| 16. | Amempigia pasi | Her/she hit him by iron. |
| 17. | Ameleta kaa | He/she brought kaa. |
| 18. | Baba Ali amewasili | Baba Ali has arrived. |
| 19. | Amekuja na nyanya | He/she has come with tomatoes. |
| 20. | Amekamata kamba | He/she has seized the cord. |
| 21. | Amevaa pamba | Wearing a cotton or pamba. |
| 22. | Issa kaleta kamba | Issa carries a string. |
| 23. | Watoto wanarushia pasi | Kids throw the cross |
| 24. | Nimenunua taa. | I have bought a lamp. |

| | | |
|---|---|---|
| 25. | Baba kaniletea gari | Dad brought me a car. |
| 26. | Juma anakopa. | Juma is borrowing |
| 27. | Asha anapanda mti | Asha climbs a tree. |
| 28. | Ameangusha paa. | He/she has broken the roof. |
| 29. | Mtoto anaendesha | The baby is driving |
| 30. | Fat-hiya anakopa | Fat-york is borrowing |
| 31. | Ameangusha paa. | He has broken the roof. |
| 32. | Kata imeanguka. | The kata has drop |
| 33. | Mtoto anachezea taa. | The baby is playing with the lamp |
| 34. | Doctor mgeni ameingia. | Anew doctor has entered |
| 35. | Mtoto anapanga. | Baby makes. |
| 36. | Kaka anaua. | Brother is killing |
| 37. | Baba Ali anakuja | Baba Ali is coming |
| 38. | Mama anawasha taa | Mother is turning the light on |
| 39. | Asha ametumwa na Rama | Asha has been sent by Rama. |
| 40. | Amina ana panda. | Amina has a panda. |
| 41. | Amini anapaa. | Amina is flying. |
| 42. | Yule anapaka. | That one blows |
| 43. | Nimeona mbono. | I have seen a vision. |
| 44. | Amekalia kiti. | He has set a seat. |
| 45. | Anampigia mpira. | He hits the ball. |
| 46. | Ile ni nyumba ya wageni. | It is an inn. |
| 47. | Niletee sahani ya kulia. | Bring me the right plate. |
| 48. | Mama anampigia pasi mwanawe. | Mom throws her baby. |
| 49. | Ua limeanguka. | The flower has fallen. |
| 50. | Amekula kalenda. | Has eaten calendar. |
| 51. | Mwalimu Haji anaendesha. | Teacher Haji runs. |
| 52. | Amenipa salamu. | He has given me a greeting. |
| 53. | Mama amenunua mkungu. | Mom bought a mist |
| 54. | Amepewa buku. | He has been given a book. |
| 55. | Jecha amenunua taa. | Sand has bought a lamp. |

| | | |
|---|---|---|
| 56. | Saidi ana pamba. | Saidi has cotton. |
| 57. | Saidi ana shuka. | Saidi has a shuck. |
| 58. | Bi harusi ameletewa gari. | The bride has been brought to the car |
| 59. | Baba alileta tai. | Father brought an eagle. |
| 60. | Fatma amepigiwa ndizi. | Fatma is banned. |
| 61. | Yoyo alipigana kwa zuwena. | Yoyo fought for zuwena. |
| 62. | Shuleni kwetu hakuna mwalimu wa Kiarabu | At our school there is no Arabic teacher. |
| 63. | Juma analia kitoto. | Juma is crying childish. |
| 64. | Mtume mtoto dukani. | Send the child to the shop. |
| 65. | Hamadi! Ameumia vibaya sana. | Hamadi has been badly injured. |
| 66. | Bi Asha anaota kila siku. | Miss Asha dream everyday. |
| 67. | Nimwagie maji nyuma. | Throw water on my back. |
| 68. | Baba amerudi kazini. | Dad is back to work |
| 69. | Khamisi ana chupa. | Khamisi has a bottle. |
| 70. | Mwenye kiti ameondoka. | The chairman has left. |
| 71. | Paka amelala jikoni. | The cat has slept on kitchen. |
| 72. | Kamba imekatika. | Therope has broke. |
| 73. | Ameula na chuya. | He/sheate raw rice. |
| 74. | Akili ni nywele. | Cleaver is hair. |
| 75. | Mzee amekula chumvi. | The old man has eaten Salt. |
| 76. | Ametoka kappa. | He is from Kappa. |
| 77. | Samaki huyu ni moto. | This fish is fire |
| 78. | Kaletwa tasa. | He brough important. |
| 79. | Mwanafunzi anatoka darasani | The student is out of the class. |
| 80. | Nimempiga kwa kulia. | I beat him for crying |
| 81. | Amekula kifungo. | He is cought. |
| 82. | Amevaa miwani. | He is wearing the class. |
| 83. | Ana mkono wa buli. | He has the biru hand. |

| | | |
|---|---|---|
| 84. | Amechungulia kaburi. | He saw the semetary. |
| 85. | Ali alikula dongo. | Ali ate the sand. |
| 86. | Alikula dawa. | He ate medicine. |
| 87. | Yumaji. | He is water. |
| 88. | Amina anakopa. | Amina is sleeping.. |
| 89. | Baba amekuja kwa gari. | Dad has come by car. |
| 90. | Panya ameuwawa na kaka. | Rat has been killed by brother. |
| 91. | Mama anameza. | Mom is schewing. |
| 92. | Vijana walikula sahani moja. | Kids ate the one plate. |
| 93. | Mama Mwajuma anaitwa | Mwajuma's mother is calling. |
| 94. | Khalid amemkatia Zuwena na Juma. | Khalid has cut Zuwena and Juma |
| 95. | Bosi aliwaingilia wafanyakazi wake. | The boss has enter his workers. |
| 96. | Huenda kama ng'ombe | He goes like bull |
| 97. | Anakula na kijiko. | He ate with spoon. |
| 98. | Anaenda mjini na baiskeli. | He goes town with bicycle. |
| 99. | Khadija anatoka na Abdalla. | Khadija is going with Abdallah. |
| 100. | Chai imeingia nzi.. | The tea has been enter the fly. |
| 101. | Nyumba imeingia nyoka. | The house has enter the snake. |
| 102. | Mwalim Asha amefariki. | Teacher Asha is dead. |
| 103. | Mwalimu Mussa hasomeshi vizuri. | Teacher Mussa is not a good teac |
| 104. | Amefika salama. | He arrived safe. |
| 105. | Mjomba anashuka. | Uncle is droping. |
| 106. | Mama amenunua mto. | Mom has brough the pillow |
| 107. | Biharusi ameletewa gari jipya. | The bride has brought a new car. |
| 108. | Wanafunzi wanachezea tai. | The students are playing with ??? |
| 109. | Usinitafutie mwanangu. | Don't find me my child. |
| 110. | Ananiharibia mwanangu. | He destroy my child. |
| 111. | Mama amenunua mkungu | Mom ha buy the banana tree. |
| 112. | Anakula wali na kuku. | He is eating rice and chicken. |

| | | |
|---|---|---|
| 113. | Amekuja kwa nauli yake. | He came with hisown transport fe |
| 114. | Shemsa ameonekana na pamba nyepesi. | Shemsa has been seen with cottor |
| 115. | Kifaru kimeletwa nyumbani. | The Bufalo has been brought hom |
| 116. | Asha ameuziwa chungu na Ali. | Asha has been sold the Port by A |
| 117. | Amejia pesa zake. | He came for his money. |
| 118. | Kombo na Jecha wanapara. | Kombo and Jecha are pararing. |
| 119. | Sipendi buibui. | I hate spider. |
| 120. | Analilia bakora. | He is crying for stick. |
| 121. | Amekunywa kupindukia. | He/she drunk too much. |
| 122. | Amepata jiko. | He get a kitchen. |
| 123. | Chukua ndoo na kata. | Take the pot and the Kata. |
| 124. | Kanunue chenza na uzile. | Go buy an orange and eat it. |
| 125. | Mama amepigwa na mwanawe. | Mother has een beeten by his chil |
| 126. | Mkaangie mwanangu. | Fry for my child. |
| 127. | Mkimbilie mgeni. | Run for the guest. |
| 128. | Baba ameleta kamba kwa mama. | Dad has brought a loap to mom. |
| 129. | Wizi wa silaha umeongezeka. | Weapon theft has been increased. |
| 130. | Nyumba imebomolewa nini? | What does the house been destroy |
| 131. | Mama anatupa. | Mother is throwing |
| 132. | Zainab yupo fujoni. | Zainab is in trouble. |
| 133. | Khamis amekuja na waridi.. | Khamis has come with rose. |
| 134. | Waite watoto wale. | Call those children |
| 135. | Mzee Makame amenivunjia nyumba yangu. | Mr Makame has broke my house. |
| 136. | Ukija niletee pamba. | Brig me cotton when you come. |
| 137. | Rafiki yangu Asma ananifahamu. | My friend Asma knows me |
| 138. | Mzazi anamsomea mwanawe. | Parent is reading for his child. |
| 139. | Aje Jumanne.. | He should come on Tuesday. |

**Kiambatanisho Na. II: Maswali ya Utafiti**

**MIONGOZO YA USAILI DODOSO NA UDURUSU WA KIMAKTABA**

**MUONGOZO WA WAHOJI KWA WATAALAMU, WAHADHIRI, WALIMU, WAFASIRI NA WANAFUNZI**

Hojaji hii inalenga kukusanya taarifa kuhusu changamoto za kutafsiri sentensi zenye tata kutoka Kiswahili kwenda

A. Taarifa Binafsi:

Umri_____________________________________

Kazi____________________

Kiwango cha Elimu_________________________ Lugha mama_____________

B. Matumizi ya lugha ya Kiswahili:

1. Utata ni nini?

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

Je, utata unajitokeza katika sentensi?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2. Orodhesha sentensi 10 zenye utata:

(i) ____________________________________________________________

(ii) ____________________________________________________________

(iii) ____________________________________________________________

(iv) ____________________________________________________________

(v) ____________________________________________________________

(vi) ____________________________________________________________

(vii) ____________________________________________________________

(viii) ____________________________________________________________

(ix) ____________________________________________________________

(x) ____________________________________________________________

3. Bainisha utata katika sentensi hizo ulizoziorodhesha

i.

a)______________________________________________________________

b)______________________________________________________________

ii. a)

________________________________________________________________

b)______________________________________________________________

iii. a)

______________________________________________________________

b)______________________________________________________________

5. Bainisha changamoto 10 zinazojitokeza katika kutafari sentensi zenye utata kutoka Kiswahili kuunda Kiingereza:

(i) __________________________________________________________

(ii) __________________________________________________________

(iii) __________________________________________________________

(iv) __________________________________________________________

(v) __________________________________________________________

(vi) __________________________________________________________

(vii)__________________________________________________________

(viii) ________________________________________________________

(ix) __________________________________________________________

(x) ________________________________________________________

6. Utata unaweza kujitokeza katika Kiswahili

Kweli (            )                                        Sikweli (          )

7. Toa utata katika sentensi zifuatazo:

i) Niletee mbuzi______________________________________________

____________________________________________________________

ii) Ananichezea mwanangu

____________________________________________

____________________________________________

iii) Amelalia uji

____________________________________________

____________________________________________

8. Bainisha sentensi 10 zenye utata katika lugha ya Kiswahili sanifu zenyechangamoto ya kitafsiri kwenda lugha ya Kiingereza.

(i) ____________________________________________

(ii) ____________________________________________

(iii) ____________________________________________

(iv) ____________________________________________

(v) ____________________________________________

(vi) ____________________________________________

(vii) ____________________________________________

(viii) ____________________________________________

(ix) ____________________________________________

(x) ____________________________________________